# Marufuku wafungwa kutumika kwa kazi binafsi

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI imepiga marufuku wafungwa kutoka magereza mbalimbali kutumika katika kazi binafsi isipokuwa kwa kufuata utaratibu unaotambulika kisheria.

Marufuku hiyo ilitangazwa jana na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Khamis Hamza Chilo, wakati wa kikao kilichojumuisha askari polisi kutoka idara zilizopo chini ya wizara ikiwapo Jeshi la Polisi, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Jeshi la Magereza, Uhamiaji na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, kilichofanyika mkoani Singida. Chilo alisema wafungwa wana taratibu zao zinazowaongoza katika mfumo wao mzima wakiwa gerezani, huku akiwaagiza wakuu wa magereza yote kufuata taratibu hizo, kwani kutofuata taratibu hizo kutasababisha baadhi ya sheria kuvunjwa.

"Kuna taarifa za uhakika kwa wafungwa kutumika katika shughuli binafsi ikiwamo kujenga nyumba za watu binafsi na kulima mashamba ya watu binafsi, nimpongeze Kamishna Jenerali wa Magereza, Suleiman Mzee, katika kipindi chake ameanza kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha jeshi linarudi katika misingi yake," alisema na kuongeza:

"Sasa tunaona magereza inaendelea kuboreka kila uchao, sisi kama serikali tunapiga marufuku matumizi binafsi ya wafungwa katika shughuli yoyote binafsi ila kwa kufuata utaratibu." Naibu Waziri Chilo aliwapa maelekezo mbalimbali zikiwamo tuhuma za rushwa kwa askari wa usalama barabarani, upelelezi wa kesi kuchukua muda mrefu, changamoto ya Vitambulisho vya Taifa na askari wa Jeshi la Zimamoto kuchelewa kufika katika matukio ya uokozi.

"Pamoja na kazi nzuri mnayofanya lazima tukae chini kwa pamoja tujitathmini ili tuweze kuona namna ya kuwasaidia Watanzania, niagize… ni marufuku kwa askari yoyote kuchukua rushwa, tunamalizana na madereva barabarani hatuendani nao kwa mujibu wa taratibu na sheria, wengine tunawabambikizia tu kesi makusudi ili waonekane tu wamefanya makosa," alisema na kuendelea:

"Tumemuona amefanya kosa mpelekeni kunakohusika, pia suala la kuwalimbikiza mahabusu katika vituo vya polisi kwa dhana ya kusubiri upelelezi ambao unachukua muda mrefu sio suala nzuri…nawaomba wapelelezi mfanye kazi yenu, ni marufuku kuwarundika mahabusu ndio maana dhamana ikawapo wapeni dhamana kwa kufuata sheria na taratibu."



Mkuu wa Wilaya ya Liwale mkoani Lindi, Sarah Chiwamba (kulia), akipokea cheti kutoka kwa Katibu Tawala wa mkoa huo, Rehema |Madenge, katika sherehe za kupongeza mkoa huo kufanya vizuri katika mtihani ya kitaifa ya shule za msingi na sekondari zilizofanyika Nachingwea juzi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Mwanafunzi, mwendesha bodaboda wauawa kinyama, miili yao yatelekezwa

Na Waandishi Wetu

WATU wasiojulikana wanadaiwa kuwaua mwanafunzi na mwendesha bodaboda katika matukio tofauti huku mwili wa mwanafunzi ukiwa na jeraha kichwani na wa dereva umetobolewa macho na kutelekezwa vichakani.

Katika tukio la mwanafunzi, imethibitika ni wa kidato cha nne Shule ya Sekondari ya Kata ya Mkolye, wilayani Sikonge, mkoani Tabora, Mwajuma Mtunda (17). Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo, Kaimu Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Mkolye, Elineus Nchimbi, alisema tukio hilo lilitokea katika kitongoji cha Kitimbasha, Kata ya Mkolye, ambalo naye alijulishwa na Mwenyekiti wa kitongoji hicho, Masulunzu Igoma.

Nchimbi ambaye ni Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mkolye, alisema baada ya taarifa hiyo siku iliyofuata wananchi walifahamishwa na kuanza kumtafuta mwanafunzi huyo ambaye walifanikiwa kuupata mwili wake ukiwa kwenye vichaka.

Alifafanua kwamba, vilevile walikuta mwili wa mwanafunzi huyo ukiwa umevuliwa nguo na kubakwa huku kisogoni akiwa na jeraha.

Alifafanua kwamba kufuatia hali hiyo, serikali ya kijiji imepanga kuitisha kikao cha dharura na baadaye mkutano wa hadhara ili waweze kujadili na kuweka mikakati ya kukomesha vitendo hivyo kutojirudia.

Mkolye alibainisha pia kwamba ili waweze kukabiliana na vitendo vya aina hiyo kinachohitajika kwa sasa ni kujenga mabweni ya wasichana katika shule za sekondari ili waweze kuwanusuru wanafunzi wa kike kutofanyiwa vitendo vya kikatili.

Kwa upande wake mzazi wa mwanafunzi aliyeuawa, Nassibu Mtunda, alisema siku ya tukio mwanawe, aliondoka nyumbani asubuhi kwenda shule, lakini hakurudi siku hiyo hadi siku ya pili mwili wake ulivyookotwa vichakani.

"Kwa kweli nimeumia sana kumpoteza mwanangu, Mwajuma kwa kuwa ameuawa kikatili sana ila mimi naiomba serikali ifanye uchunguzi wa kina ili kuwabaini waliohusika na unyama huo wa kikatili," alisema huku akibubujikwa na machozi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Kamishna Msaidizi, Safia Jongo, alikiri kuwapo kwa tukio hilo la mauaji ya mwanafunzi na aliuawa kwa kupigwa na kitu kizito kisogoni.

Alisema Jeshi la Polisi limefanya upelelezi wa kina na kubaini kuwa mwanafunzi huyo alikuwa na mpenzi wake mmoja ambaye hakumtaja jina na baada ya kutengana naye, aliamua kutafuta mpenzi mwingine ambaye naye hakumtaja jina lake.

Alisema kwamba baada ya kijana huyo kuona mwanafunzi ana kijana mwingine ndipo alipoamua kumtishia maisha, lakini hata hivyo wazazi wake hawakutoa taarifa hiyo Kituo cha Polisi Sikonge au kwenye uongozi wa kitongoji au kwa Ofisa Mtendaji wa kijiji au kata.

Alisema baada ya kutokea kwa mauaji hayo kijana huyo alitoroka kwenda Wilaya ya Sumbawanga, mkoani Rukwa hadi hivi sasa wanaendelea kumtafuta na baadhi ya vijana waliowahoji waliwaachia huru baada ya kubaini hawajahusika na mauaji hayo na kuongeza kuwa mwanafunzi aliuawa kwa kupigwa na kitu kizito kisogoni.

Kamanda Jongo, aliitaka jamii katika wilaya zote za Mkoa wa Tabora kuacha kufanya vitendo vya mauaji na badala yake wananchi wawe na hofu ya Mungu kwa kuwa na matendo mema huku akiahidi kuendelea na kutoa elimu kwa wananchi ili waache kujichukulia sheria mkononi.

Aidha, katika tukio la kuuawa mwendesha pikipiki, mkazi wa Kijiji cha Nyangao 'A' Halmashauri ya Mtama, Mkoa wa Lindi, Mustafa Mtumwiche, inadaiwa kuuawa kikatili na watu wasiojulikana na mwili wake ukitelekezwa maeneo ya Kijiji cha Mtakuja, huku shingo yake ikiwa imevunjwa.

Taarifa zilizothibitishwa na mashuhuda wa mwili huo na viongozi wa serikali, akiwamo Mwenyekiti wa Kijiji cha Nyangao 'B' ambacho bodaboda huyo alikuwa akifanyia shughuli zake za kusafirisha abiria, zinaeleza Mtumwiche alifariki wiki moja iliyopita.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Nyangao 'B', Erick Elias Lukanga, alipoulizwa kuhusu kifo hicho, alikiri kutokea na mwili wake kukutwa umetelekezwa eneo la Kijiji cha Mtakuja, huku shingo ikiwa imevunjwa na macho yake yakiwa yametobolewa.

Alisema kabla ya mwili wake kupatikana, Mtumweche kwa muda wa wiki mbili hakuonekana nyumbani kwao, kitendo kilichomfanya baba mkwe wake kwenda Kituo cha Polisi Nyangao kutoa taarifa.

Lukanga alisema baada ya kutoa taarifa hiyo, ndugu, jamaa, majirani na viongozi wa vijiji husika walianza kumtafuta maeneo mbalimbali ya Mtama bila mafanikio.

Alisema wakiwa wanaendelea kutafakari, siku ya Jumatano saa sita mchana, wiki iliyopita, walipata taarifa kuonekana kwa mwili wake ukiwa umetelekezwa pembezoni mwa barabara eneo la Kijiji cha Mtakuja 'B' na Nyangao 'B'.

"Mimi ni miongoni mwa watu tulioshiriki kumtafuta na tukafanikiwa mwili wake kuukuta eneo la Kijiji cha Mtakuja 'B' na Nyangao 'B, huku shingo imevunjwa na macho kutobolewa," alisema Lukanga.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, ACP Mtatiro Kitinkwi, alithibitisha kutokea kwa kifo hicho na kueleza jeshi hilo linaendelea kuwasaka waliohusika na mauaji hayo ili sheria ichukue mkondo wake.

●**Imeandikwa na Jumbe Ismailly, SIKONGE na Said Hamdani, LINDI**

HABARI KITAIFA

# Samia kuongoza mkutano wa uwekezaji

**Na Lulu George,** TANGA

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kuwa mwenyekiti wa mkutano wa uwekezaji na biashara kwa wadau wa ndani na nje ya nchi, ikiwa ni hatua ya kutangaza fursa za kiuchumi zilizopo kwenye mkoa wa Tanga.

Katika mkutano huo unaotarajiwa kufanyika Machi 18, mwaka huu, pia utafanyika uzinduzi wa kitabu maalum kwa ajili ya kutangaza fursa za uwekezaji za mkoa wa Tanga.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martine Shighela alisema Makamu wa Rais ataanza ziara ya kikazi leo mkoani humo na kuhitimisha Machi 19.

Shigela alisema katika ziara hiyo atakagua miradi mbalimbali ya maendeleo katika wilaya za Korogwe, Handeni, Mkinga, Muheza, Pangani na Tanga.

"Makamu wa Rais atatembelea viwanda mbalimbali ikiwamo vya usindikaji wa vyakula na kupata fursa ya kuzungumza na wananchi wa Tanga kupitia mikutano ya hadhara, ila kubwa zaidi ni huu mkutano wa uwekezaji unaotarajiwa kufanyika jijini hapa," alisema.

Aliwataka wakazi wa mkoa huo kujitokeza kwa wingi ili waweze kujua masuala mbalimbali yanayohusu mustakabali wa mkoa wao.

"Tanga tuna fursa mbalimbali za kiuchumi ikiwamo mpaka, bahari, reli, uwanja wa ndege na barabara, hivyo kwa mwekezaji yeyote anayetarajiwa kuja kuwekeza hapa ni nafasi nzuri sana kwake na hatajutia miundombinu yote ipo na ni ya uhakika," alisisitiza.

Mkutano huo wa uwekezaji na biashara ujumbe wake ni 'Tanga Kitovu cha Uwekezaji na Biashara, Afrika Mashariki'.

# Wadai kulazimishwa kununua barakoa hata wasipozivaa

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WANANCHI wilayani Nyamagana, mkoani Mwanza, wamelalamika kuuziwa barakoa kwa lazima katika lango kuu la kuingia ofisi ya Mamlaka ya Mapato Mkoa wa Mwanza (TRA), wanapokwenda kupata huduma.

Wakizungumza na Nipashe wananchi hao walidai wakinunua barakoa hizo hata wasipozivaa wanaruhusiwa kuingia ndani na kupata huduma.

"Tunaomba suala hili la uvaaji wa barakoa katika ofisi ya TRA Mwanza lipatiwe ufumbuzi maana inaonyesha wazi ni kama mradi wa watu, mteja anapofika getini hawezi kuingia bila barakoa inambidi anunue, kama hana hela basi siku hiyo hawezi kupatiwa huduma, kinachoshangaza ukinunua tu unaruhusiwa kuingia ndani ya ofisi hiyo inakuwa ni hiari yako uvae au usivae," alisema Shenda Marashi.

Akizungumzia madai hayo, Meneja wa TRA Mkoa wa Mwanza, Joseph Mtandika, alisema mamlaka hiyo imejiwekea utaratibu huo wa mteja kuvaa barakoa kabla ya kuingia ndani kupata huduma yoyote.

"Hicho wanacholalamikia wananchi sio kweli, sisi tunachukua tahadhari ya magonjwa ya milipuko ikiwamo corona maana unaambiwa akili yako changanya na ya kuambiwa hivyo tumeweka mabango na hakuna mtu ambaye anapata huduma bila kuvaa barakoa, kunawa mikono na kujipaka vitakasa mikono," alisema Mtandika.

# Mil.161/- zanunua mashine za kisasa

**Na Hamisi Nasri, MASASI**

HOSPITALI ya Mkomaindo Halmashauri ya Mji wa Masasi mkoani Mtwara, imenunua mashine tatu za kisasa ikiwamo ya mionzi (X-ray) kupitia mkopo wa Bima ya Taifa ya Afya (NHIF) zenye thamani ya Sh. milioni 161.

Mashine hizo ni kwa ajili ya kuboresha huduma za afya hospitalini humo. Kaimu Mganga Mkuu wa halmashauri hiyo, Peter Majura, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na gazeti hili.

Alifafanua kuwa zimenunuliwa kwa fedha za mapato ya ndani ya hospitali hiyo, mkopo huo utakuwa ukilipwa kupitia makubaliano ya mkataba kati ya NHIF na uongozi wa hospitali hiyo.

Alizitaja mashine hizo ni X-ray, mashine ya usingizi kwa ajili ya mgonjwa anapofanyiwa upasuaji mdogo na ya kutakasa vifaa tiba vinavyotumiwa na madaktari wakati wa kutoa huduma za afya.

Majura alieleza kwamba kwa upande wa mashine ya X-ray iliyonunuliwa ina uwezo mkubwa wa kutoa huduma kwa wagonjwa wapatao 200 kwa siku, ukilinganisha na uwezo wa mashine ya zamani iliyopo.

Aidha, alisema kwa sasa mashine hizo zitakuwa zikitumika kwa pamoja ili kuongeza ufanisi wa upatikanaji wa huduma hiyo ambayo awali ilikuwa ikipatikana kwa shida.


KCB BANK

"THE CITIZEN RISING WOMAN AWARDS"

Katika kusherehekea siku ya mwanamke Duniani - Jumatatu Machi 8, 2021, KCB Bank Tanzania ilipokea Tuzo ya "the Citizen Rising Women" katika kitengo cha "Woman of the Future 2021 "; iliyoandaliwa na Mwananchi Communications Limited na mchakato wa uteuzi kufanywa na KPMG.

Visababishi vya ushindi huu ni pamoja na:
- Program ya KCB 2jiajiri ya kuwawezesha kiuchumi na kifedha wanawake na vijana nchini.
- Kuwepo kwa sera zinazohakikisha usawa wa kijinsia na ushirikishwaji wa kifedha.
- Kuwepo kwa sera zinazopinga aina yoyote ya unyanyasaji mahali pa kazi.
- Mpango wa kushauri na kukuza viongozi wa kesho wanawake.
- Chumba maalum kwa ajili ya unyonyeshaji na wanawake wajawazito.




Mkuu wa Masoko, Mawasiliano na Uhusiano wa Benki ya KCB Tanzania, Christina Manyenye, akipokea tuzo ya "The Citizen Rising Woman" katika kitengo cha "Woman of the Future 2021" kulia kwake ni Mkuu wa Rasilimali Watu wa KCB Bank Tanzania, Fauqiya Shareef na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa KCB Bank Tanzania, John Ulanga iliyokabidhiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo - Abdallah Ulega aliyekuwa mgeni rasmi pembeni yake akiwemo na Mkurugenzi Mtendaji wa Mwananchi Communications Ltd, Bakari Machumu kwenye hafla ya siku ya Wanawake Duniani iliyoandaliwa na Mwananchi Communications Limited.





Mkuu wa Masoko, Mawasiliano na Uhusiano wa KCB Bank Tanzania, Christina Manyenye akishikilia tuzo ya "the Citizen Rising Woman" katika kitengo cha "Woman of the Future 2021" . Kulia kwake ni Mkuu wa Rasilimali Watu wa KCB Bank Tanzania, Fauqiya Shareef na wafanyakazi wa Idara ya Masoko, Mawasiliano na Uhusiano.

# Wanafunzi wakaa chini kisa wazazi kugomea kuchangia madawati

**Na Daniel Limbe,** CHATO

WAKAZI wa Kata ya Chato, wilayani Chato, mkoani Geita, wanadaiwa kugomea utaratibu wa kuchangia madawati ya wanafunzi wa kidato cha kwanza wanaokaa chini.

Msimamo huo ulitolewa mwishoni mwa wiki, kwenye kikao cha wazazi wenye watoto wanaosoma kidato cha kwanza Shule ya Sekondari Chato, muda mfupi baada ya kutakiwa kuchangia madawati kwa ajili ya kuondoa uhaba, jambo ambalo lililopingwa na wazazi hao.

Kikao hicho kiliitishwa na Diwani wa Kata ya Chato, Mange Sayi, ambaye pamoja na mambo mengine aliwaomba wazazi hao kusaidia jitihada za serikali kuboresha miundombinu na mazingira ya kusomea watoto kwa kukubali kuchangia madawati.

Pia aliwaeleza wazazi hao kuwa wanafunzi 160 kati ya 473 waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza 2021/22, wanakaa chini kutokana na upungufu wa madawati.

Baada ya maelezo hayo, wazazi hao walipinga ombi hilo kwa madai linakiuka miongozo na maelekezo ya Rais John Magufuli, aliyetaka elimu itolewe bure na kwamba kukiwa na wazazi walioguswa na suala la uchangiaji elimu michango yao waipeleke kwa wakurugenzi watendaji wa halmashauri husika.

Wakizungumza na gazeti hili, baadhi ya wazazi Lucas Masai na Philipo Butondo, walidai kuchangishwa madawati ni sawa na kupingana na maelekezo ya Rais Magufuli, jambo ambalo halistahili.

"Tumeshangazwa sana na kauli za viongozi wetu kutaka kuchangia madawati...jukumu ambalo limekuwa linatekelezwa na serikali kuhakikisha madarasa na madawati yanapatikana ili wanafunzi wapate elimu kwa ubora," alisema Butondo.

Wamedai ili kukabiliana na tatizo hilo kuna haja kwa serikali kuruhusu wanafunzi hao kusoma kwa kupokezana (asubuhi na mchana) hatua itakayosaidia wote kukaa kwenye madawati badala ya kushinikiza wazazi.

Mpaka kikao kinamalizika hakuna mwakilishi wa mkuu wa shule wala mtendaji wa kata hiyo aliyeonekana.

# RC awasilisha ombi huduma dharura Hospitali ya Tumbi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Evarist Ndikilo, amewasilisha maombi ya uwapo wa huduma za dharura katika Hospitali ya Rufani ya Tumbi kwa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa.

Ndikilo aliwasilisha maombi hayo juzi mjini Kibaha kwa Kamati hiyo ilipofanya ziara ya kukagua mradi wa ukarabati wa Sekondari Kongwe ya Kibaha na kutembelea Hospitali ya Tumbi kujionea shughuli zinazofanywa.

Alisema endapo zitakuwapo huduma za dharura katika hospitali hiyo, itasaidia kupunguza msongamano katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na tawi la Mloganzila.

"Hii hospitali yetu ipo katika barabara kuu ya Chalinze-Morogoro ni lango la kuingia na kutokana nchi jirani huduma za kiafya zinatakiwa ziboreshwe sio kukimbiza katika Hospitali ya Muhimbili, lakini utaratibu wa huduma za dharura ulianza itasaidia wagonjwa wanaotakiwa kwenda Hospitali ya Taifa kuishia hapa hapa," alisema.

Alisema mfumo wa ukusanyaji fedha unaofanywa kwa sasa umeongeza mapato kutoka Sh. 300,000 kwa siku hadi Sh. milioni tatu.

Mbunge wa Jimbo la Kibaha Vijijini, Michael Mwakamo, aliomba kupatiwa upya gharama wanazotozwa wagonjwa ambao hawakufika hapo kwa kupewa rufani.

Kwa mujibu wa mmoja wa wataalamu wa hospitali hiyo, Radigunda Chuwa, mgonjwa anayefika hapo kwa kupewa rufani kadi yake ni Sh. 2,500 huku aliyefika bila kupata rufani kadi yake akikatiwa kwa Sh. 5,000 ambayo imelalamikiwa na mbunge huyo kuwa inamuumiza mwananchi.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Humphrey Polepole, alisema viongozi na watoa huduma wa afya wanatakiwa kutoa elimu kwa wananchi kuanza kupata huduma za afya kwenye ngazi ya zahanati na vituo vya afya badala ya kukimbilia hospitali za rufani.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Serikali za Mitaa, David Silinde, alisema mpango wa serikali ni kuhakikisha kila wananchi anatumia bima ya afya.

Silinde alisema mapendekezo yote yaliyotolewa na kamati hiyo yamepokelewa na yatafanyiwa kazi.




Meneja wa Chaneli za Kidijitali na Malipo kwa Mtandao M-Pesa wa Kampuni ya simu za mkononi ya Vodacom Tanzania PLC, Josephine Mushi (kulia), akipokea tuzo za Tanzania Digital Awards kutoka kwa Ofisa Uendeshaji wa Kampuni ya Serengeti Bytes, Michael Mallya, Vodacom imeshinda tuzo mbili, na (App) bora ya huduma za kifedha kupitia M-Pesa App na kampeni bora ya masoko mtandaoni, kampeni ya "Yajayo Yanafurahisha" ilishinda. Hafla hiyo ilifanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kahama kinara matukio ya ukatili wa kijinsia

**Na Mohab Dominck,** KAHAMA

WILAYA ya Kahama, mkoani Shinyanga imetajwa kuwa kinara wa matukio ya ukatili wa kijinsia kwa watoto ikiwamo kutokwenda shule kutokana na kuajiriwa katika mazingira hatarishi na kuishi maisha ya hatari.

Ilibainishwa kuwa watoto wengi wanafanya kazi katika mazingira hatarishi huku wengine wakihangaika mitaani kwa ajili ya kujipatia riziki na fedha za kuwasaidia katika maisha yao ambayo hayana furaha.

Kamishna Mkuu Msaidizi wa Skauti nchini kutoka makao makuu, Omary Mavura, alisema hayo wakati akitambulisha mradi mpya wa ulinzi na usalama wa watoto ambao umefadhiliwa na Makao Makuu ya Shatu Afrika yalioko nchini Kenya, ambao utajumuisha wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, wilayani Kahama.

Mavura alisema katika maandiko 12 yaliondikwa ya kuomba miradi katika makao makuu ya skauti, mradi mmoja pekee wa ulinzi na usalama kwa watoto ulioombwa na Wilaya ya Kahama ulikubaliwa na kutekelezwa kwa mwaka mmoja katika shule za msingi na sekondari.

Alisema pia Shirika la Nyumba la Taifa limesaidia kuhakikisha mradi huo unatekelezwa kwa ufasaha katika Wilaya ya Kahama na kuongeza imani ya kupata mradi mwingine kwa ajili ya siku za baadaye.

Alisema suala la ulinzi na usalama kwa watoto ni kazi ya mzazi, sio katika shule na kuongeza kuwa lazima ajue kitu ambacho mtoto anakifanya kwa siku na kuonya wasiwaachie walimu shuleni kwa kuwa hata wao wana kazi nyingi.

Mratibu wa mradi huo, Kenedy Alphonce alisema lengo kuu la mradi huo ni pamoja na kuisaidia serikali katika mapambano ya kupunguza ukatili kwa watoto na kuelimisha jamii juu thamani ya kutunza watoto wao.

Naye Glory Peter, mmoja wa wanufaika na mradi huo, ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha sita katika Shule ya Sekondari ya AbdulRahim Busoka, alisema mafunzo watakayopewa yatawasaidia kujiamini watoto na kuwajengea hali ya uzalendo kwa taifa.

Alisema kupitia skauti watajipatia ajira binafsi na kuondokana na dhana ya wanafunzi kusoma na kutegemea ajira kutoka serikalini na kusahau kuwa wanaweza kutumia elimu ya kujitegemea ambayo itatokana na mafunzo wanayopata.

Mgeni rasmi katika ufunguzi wa mradi huo aliyemwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, ambaye ni Katibu Tarafa ya Kahama Mjini, Julius Chagama, alisema mradi huo umekuja katika wakati muafaka na kuwataka wanafunzi kuhakikisha kuwa wanautendea haki na serikali ipo nyuma yao katika kupinga ukatili wowote unafanyika kwa watoto kama udhalilishaji wa kuwabaka, kuwalawiti ambao umeshika kasi nchini.

**HABARI KITAIFA**

# Mkulima mbaroni tuhuma za uzushi JPM kuumwa

**Na Francis Godwin,** IRINGA

JESHI la Polisi mkoani Iringa, limemkamata mkulima wa kijiji cha Kibengu, Wilaya ya Mufindi mkoani hapa, Augustino Kiliwa (26), kwa tuhuma za kuchapisha kwenye ukurasa wake wa Facebook taarifa za uzushi za kuumwa kwa Rais Dk. John Magufuli.

Msaidizi wa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Iringa, Rienda Millanzi, alisema mtuhumiwa huyo alichapisha taarifa hizo Machi 11, mwaka huu, kwenye ukurasa wake huo kinyume na sheria. "Aliandika ujumbe ambao ulileta taharuki na wenye mihemko ndani ya jamii kuhusu afya ya Rais Magufuli," alisema Malliza aliyezungumza kwa niaba ya Kamanda wa mkoa huo, Juma Bwire.

Alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa Machi 13, mwaka huu, majira ya saa saba mchana katika kijiji cha Kibengu, kupitia kikosi maalum cha polisi kinachoshughulikia na makosa ya mtandao.

Pia alisema upelelezi wa tukio hilo unaendelea na baada ya kukamilika mtuhumiwa atafikishwa mahakamani kujibu tuhuma hizo. Kwa mujibu wa kamanda, Jeshi la Polisi litaendelea kuchukua hatua kali kwa kuwakamata wanaosambaza taarifa za uongo sio kwa Rais Magufuli, bali zozote zitakazobainika ni za uongo.

Kadhalika, jeshi hilo limewataka wananchi kujiepusha na kuchapisha ama kusambaza mitandaoni taarifa ambazo hawana mamlaka nazo kwa kuwa kwa kufanya hivyo ni kinyume cha kifungu namba 14 cha Sheria ya Makosa ya Mtandaoni.

# Wananchi washangaa mwekezaji kuzuiwa kuchonga barabara

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

BAADHI ya wakazi wa Kijiji cha Nyambura, mkoani Shinyanga wamesikitishwa na mvutano wakati wa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo inayowasaidia wananchi.

Wananchi hao wamesema baadhi ya viongozi wa kisiasa wanazuia wawekezaji kuwasaidia hata kuchongewa barabara ambazo hazipitiki.

Walidai hivi karibuni diwani wao Kamuli Mayunga, alimzuia mwekezaji wa kiwanda cha kukoboa mpunga kuwachongea barabara iliyokuwa haipitiki kwa kipindi kirefu.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Mabao Investment and General Pets Control Ltd (AMJ), Abel Thomas, alijitolea kuchonga barabara hiyo yenye urefu wa kilomita mbili kwa kutumia greda lake ili kuwarahisishia usafiri kwa wananchi hao.

Jumanne Mhoja ambaye ni mkazi wa eneo hilo, alipinga hatua hiyo ya diwani kuzuia kuchongwa barabara hiyo kwa kuwa kazi aliyokuwa akiifanya ni ya kujitolea ili kuwasaidia wao.

Hata hivyo, Diwani Mayunga akijibu tuhuma hizo, alisema hapingi maendeleo bali alichomkataza dereva wa greda aliyekuwa akichonga barabara ni kumtaka asifike kukwangua eneo lake na kuegemea upande mmoja.

Kwa upande wake, Magdalena Mhoja, mkazi wa kata hiyo alisema diwani huyo hakupaswa kumzuia mwekezaji kuchonga barabara kutokana na sababu yoyote kwa kuwa walikuwa wanateseka kwa kupita barabara mbovu.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Omary Nkindwa, alisema serikali ya kijiji haizuii maendeleo kwa wananchi wake na kwamba mwekezaji huyo anapaswa kupongezwa.

"Tumependekeza Wakala wa Barabara Vijijini na Mjini (TARURA), wawe tayari kujitokeza na kuonyesha mipaka ya barabara ili migogoro inayoweza kujitokeza kwa kuwa viwanja vingi vya watu havijapimwa," alisema Nkindwa.

Meneja wa TARURA katika Manispaa ya Kahama, Joab Mutawaba, alipongeza msaada huo wa mwekezaji na kwamba waliruhusu afanye kazi hiyo.

# DC atangazia vita wanaouchafua mji

**Na Happy Severine,** BARIADI

MKUU wa Wilaya ya Bariadi, Festo Kiswaga, amewaonya mama lishe na watu wanaotiririsha maji machafu kwenye mitaro ya barabara, huku akitangaza kuwachukulia hatua maofisa afya wanaozembea kusimamia suala la usafi katika maeneo yao.

Alitoa onyo hilo mwishoni mwa wiki kwenye kikao cha Ushauri cha Wilaya (DCC), kilichokutanisha watendaji katika Halmashauri ya Bariadi mkoani Simiyu.

Alisema wanaendelea kushughulikia baadhi ya wananchi wanaochafua mazingira na mitaro iliyojengwa na serikali kwa gharama kubwa.

Kiswaga aliwaonya wafanyabiashara na mama lishe wanaotiririsha maji machafu yanayosababisha mji wa Bariadi kuonekana mchafu, licha ya serikali kujenga na kuweka taa za barabarani kwa lengo la kuboresha mazingira.

"Niwaonye maofisa afya na watendaji nitakapokagua na kukuta mtaro au kwenye nyumba yoyote au nyumba ya kulala wageni au ya biashara basi ofisa afya nitakuchukulia hatua, na wewe unayetiririsha maji machafu nitakuchukulia hatua," alisema Kiswaga.

Alisema atawashtaki wale wanaochafua mazingira kwa sheria ya mazingira na kuwataka maofisa mazingira kufanya kazi kwa mujibu wa sheria.

Aliongeza kuwa Mji wa Bariadi ni makao makuu ya Mkoa wa Simiyu, na kwamba baadhi ya watu wanaishi kama wako wilayani, huku akisema kuanzia sasa amerudisha operesheni ya kukagua usafi kila Alhamisi ya mwisho wa mwezi.

"Nitashiriki mimi mwenyewe pamoja na kamati ya ulinzi na usalama kukagua hali ya usafi katika Mji wa Bariadi ili uwe katika hali ya usafi, nataka safari hii tushike namba moja katika usafi, na hatuna sababu ya kuwa na mji mchafu wakati serikali imeshatoa fedha kwa ajili ya kutengeneza barabara," alisema Kiswaga.

Aliongeza kuwa Rais John Magufuli ameshatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara na uwekaji wa taa za barabarani pia ameshatoa fedha kwa ajili ya ununuzi wa magari matatu ya kuzolea taka ngumu na majitaka, lakini bado baadhi ya watu wanachafua mazingira.

## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZ0 LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **GADAU AUCTION AUCTION MART AND COMPAY LTD, LOCUS DEBT MANAGEMENT LTD na MAK RECOVERIESLTD**, Kwa idhini tuliyopewa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD** tunatoa muda wa siku 14 kwa wadaiwa walioorodheshwa kwenye jedwali hapo chini wawe wamelipa madeni wanayodaiwa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD,** Kinyume na hapo tutalazimika kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara mali walizoweka kama dhamana ya mkopo. Tarehe za kufanya minada zitatolewa kwa njia ya vipeperushi na magari ya matangazo kwenye sehemu dhamana zilipo.

| | Gadau Auction Mart & Company Limited | | |
|---|---|---|---|
| S/N | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
| 1 | Barick Joseph Idawa | Nyumba | - Ramadhani Njombe Mjini |
| | | nyumba | - Mgendela Njombe |
| 2 | Plasido D. Maulaga | Nyumba na Gari | - Kahawa Njombe |
| 3 | Gaston D. Mbavile | Nyumba Na Dhamana Nyingine | -Msete Njombe |
| 4 | Godlove Joseph Mwalongo | Nyumba | -Mgendela Njombe |
| 5 | Ezekia S Nyunja | Nyumba(Dhamana Nyingine) | - Kibena Hospital Njombe Mjinni |
| 6 | Jacob Japhet Fungilwa | Nyumba | -Igima Njombe Vijijini |
| 7 | Nebchard Charles Msigwa | Nyumba | - Ramadhani Njombe |
| 8 | Noel Emmanuel Luhoha | Nyumba | - Ramadhani Njombe |
| 9 | Samwel Isaac Mgaya | Kiwanja | -Kihesa Njombe |
| | Locus Debt Management Ltd | | |
| | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
| 10 | Leonsi A Massawe | Nyumba na Gari | -Mabogoni Moshi |
| 11 | Novath I Lyimo | Nyumba | -Uchira Moshi |
| 12 | Ambrosia R Munuo | Kiwanja | -Sanya Juu Moshi |
| 13 | Sprian George Chuwa | Viwanja Viwili | -Orio Kahe Na Mji Mpya Moshi |
| | | | |
| | Mak Recoveries Ltd | | |
| | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
| 14 | Grace Charles Longo | Nyumba ( Dhamana Nyingine) | -Makulu Dodoma City |
| 15 | Olga R Kasinde | Nyumba ( Dhamana Nyingine) | -Area C Dodoma City |
| 16 | Sarah J Ramadhan | Kiwanja(Dhamana Nyingine) | Maganga West Area Dodoma City |
| 17 | Sospeter Lazaro Lenjole | Gari | Dodoma City |
| 18 | Genovefa Proches Shayo | Kiwanja | Dodoma City |
| 19 | Juma Jafari Tongo | Kiwanja | Dodoma |
| 20 | Elieza Joseph Mwaluko | Kiwanja Na Nyumba(Dhamana Nyingine) | Mpwapwa |
| 21 | Lisungu Caswel Mahinya | Kiwanja Na Vitu Vya Biashara | Mwana Kianga- Mpwapwa |
| 22 | Baraka Patrick Mlongwa | Kiwanja( Dhamana Nyingine) | Ilolo -Mpwapwa |
| 23 | Musa Yoram Nhayo | Vitu Vya Ndani Na Biashara | Mpwapwa |
| 24 | Ibrahim Laurent Mpande | Kiwanja Plot No 2 Block B | Ujenzi Mnyakongo Kongwa |
| 25 | Silivia Yoram Nhayo | Nyumba(Vitu Vya Ndani) | Mpwapwa |
| 26 | Frank David Tegemea | Nyumba | Dodoma Mjini |
| 27 | George C Tungu | Nyumba( Vitu Vya Ndani, Biashara) | Mlalai- Kongwa |
| 28 | Mendrad P Nyakulima | Nyumba(Vitu Vya Ndani) | Chigongwe-Dodoma |
| 29 | Patrick Yoram Nhayo | Nyumba | Mpwapwa Mjini |
| 30 | Mtwaliki S Kidunda | Nyumba | Engusero-Kibaya |
| 31 | Dominick D Kiromba | Nyumba(Vitu Vya Ndani) | Ihumwa- Dodoma |
| 32 | Wilson A Ngemera | Kiwanja (Vitu Vya Ndani) | Bahi & Dodoma City |
| 33 | Oberlin K. Swai | Nyumba (Vitu Vya Nyumbani) | Mlimwa C – Dodoma City |

### MASHARTI YA MNADA

1. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
3. Mnunuzi atayeshinda anapaswa kulipa 25% ya bei aliyofikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia atalipa ndani ya siku kumi na nne(14) toka tarehe ya mnada, Kinyume na hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha Hati miliki(Transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa ni la mnunuzi.
5. Mnada utafanyika mahali ambapo dhamana zilipo na si vinginevyo.

KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA NAMBA

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Gadau Auction Mart And Company L.T.D**
**S.L.P 40855, Dar Es Saalam**
**Simu; 0714 635599/ 0785 636864**

**Na Mkurugenzi Mtendaji,**
**Locus Debt Management Ltd**
**Crispin T. Meela**
**0756 – 140199/0784 – 140199**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba onyesheni mnaweza bila mashabiki kwa Mkapa

**BAADA** ya kucheza mechi tatu, mbili ugenini bila mashabiki na moja nyumbani ikiwa na mashabiki wake, hatimaye Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), limeagiza kuanzia sasa mashabiki wa klabu ya Simba nao hawataruhusiwa kuingia uwanjani kuishuhudia timu yao kwenye mechi zake za Ligi ya Mabingwa Afrika.

Awali, CAF iliruhusu mashabiki wa Simba kuingia kwa asilimia 50 ya uwezo wa uwanja ambao ni sawa na 30,000, katika mechi zake za nyumbani kutokana na Tanzania kutokuwa na tishio kubwa la maambukizo ya virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19.

Hatua hiyo iliipa Simba nafasi kubwa ya kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Al Ahly ya Misri zilipokutana Uwanja wa Benjamin Mkapa, jambo ambalo pia lililalamikiwa na Kocha Mkuu wa timu hiyo, Pitso Mosimane, kuwa ilikuwa moja ya sababu ya timu yake kupoteza mchezo huo.

Mosimane alikwenda mbali zaidi kwa kudai kwamba hakuna usawa kwa kuwa timu nyingine nyumbani mashabiki hawaruhusiwi kuingia uwanjani, lakini kwa Simba yenyewe inapata sapoti kubwa kutoka kwa mashabiki wake kutokana na ruhusa hiyo.

Pamoja na kwamba mashabiki kweli ni sawa na mchezaji wa 12 uwanjani, tunatambua Simba itakuwa imepoteza nguvu kubwa kutoka kwao ambao wamekuwa mstari wa mbele kwenda uwanjani kuisapoti kila inapocheza husuan mechi za kimataifa.

Lakini hilo halitupi mashaka makubwa kutokana na ukweli kwamba, Simba imeweza kuvuna pointi nne nje ya Uwanja wa Benjamin Mkapa katika mashindano hayo msimu huu baada ya kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya AS Vita nchini DR Congo kabla ya kwenda Sudan kulazimisha sare tasa dhidi ya Al-Merrikh, mechi zote hizo zikichezwa bila mashabiki.

Hivyo, kama Simba imeweza kwenda ugenini na kushinda na kisha kutoka sare, tunaamini kabisa endapo wachezaji wakiamua kujituma na kutambua umuhimu wa kulinda rekodi yao ya kutopoteza nyumbani, hata bila mashabiki inaweza kupata ushindi tena mkubwa.

Kikubwa kinachotakiwa kwa viongozi na benchi la ufundi la Simba, ni kuwajenga kisaikolojia wachezaji wao, watambue kuwa ingawa wakigeuka jukwaani hawatawaona mashabiki wao, lakini wapo pamoja nao na watakuwa wakiwaunga mkono na kuwashabikia wakiwa nje ya uwanja na kila pembe ya nchi kama ilivyo kawaida yao.


Lakini mashabiki hawana budi kuonyesha kuwa wapo pamoja na wachezaji wao, angalau hata kwa kuwa katika kumbi za starehe na baa zilizopo nje ya Uwanja wa Benjamin Mkapa, kushuhudia mechi hiyo kupitia luninga na kushangilia kwa nguvu zote, kelele ambazo tunauhakika zitawafikia wachezaji wakiwa Uwaja wa Mkapa wakati wakiendelea na mechi yao kesho dhidi ya Al-Merrikh.

Kama ambavyo, tunatambua mchezo huu ni wa muhimu kwa Simba kushinda ili kujiweka katika nafasi nzuri zaidi ya kufuzu robo fainali, wachezaji pia hawana budi kulibeba hilo kichwani na kuingia uwanjani wakiwa na morali ya juu ya ushindi zaidi hata wakati wakiwa na mashabiki wao.

Nipashe hatuoni sababu yoyote ya kuizuia Simba kupata ushindi kesho, ingawa tunatambua wazi wachezaji watakosa sapoti kubwa waliyoizoea kutoka kwa mashabiki wao jukwaani.

Tunaitakia kila la kheri Simba kuelekea mchezo huo wa kesho, kwani lengo letu ni kuiona ikifika mbali zaidi kwenye michuano hiyo ili kuiongezea Tanzania pointi zitakazoiwezesha kuingiza timu nne kwenye mashindano hayo ya CAF msimu ujao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Simba wawekeeni mashabiki runinga Uwanja wa Uhuru kuwaliza Merrikh

Na Adam Fungamwango

**KILA** kona ukipita utakuta mashabiki wa klabu ya Simba wanasononeka kutokana na kutoruhusiwa kuingia tena Uwanja wa Benjamin Mkapa kwenye mechi yao ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa kesho kati yao na Al-Merriekh ya Sudan.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo juzi alisema wamepokea maagizo kutoka Shirikisho la Soka Afrika (CAF), likiwataarifu kuwa mechi zote zilizobaki za ligi hiyo zitachezwa bila mashabiki, kuanzia na mechi hiyo ya kesho.

Huko nyuma, Simba imecheza mechi dhidi ya Plateau ya Nigeria, Platinum ya Zimbabwe, na Al Ahly ya Misri ikiwa na mashabiki ambao walitakiwa wasidizi asilimia 50 ya uwezo wa uwanja.

Kumekuwa na dhana mbalimbali kutoka kwa mashabiki wengine wakidai kuwa ni zengwe la baadhi ya timu zinazoshiriki michuano hiyo baada ya kuona huenda Simba inapata faida sana inapokuwa inashangiliwa na wafuasi wake, tofauti na nchi zingine ambazo zinakuwa hazina mashabiki kabisa.

Lakini baadhi wanasema CAF wamefanya hivyo ili kuleta usawa kwa timu zote, wengine wakisema wamefanya hivyo kwa ajili ya kuchukua tahadhari kutokana na magonjwa mbalimbali ya kupumua.

Vyovyote itakavyokuwa, mashabiki wa Simba nchini Tanzania wamekuwa na mchango mkubwa kwa timu yao. Wamekuwa wakishangilia na kuchagiza timu yao kupata ushindi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Hilo lilimtisha hadi Kocha Mkuu wa Al Ahly ya Misri, Pitso Mosimane, na baadaye akaeleza hisia zake kuwa mashabiki wa Simba kwa kiasi kikubwa walichangia timu yake kupoteza kwa jinsi walivyokuwa wakishinikiza, lakini akalalamika kuwa hakuna usawa, kwani wao wanacheza nyumbani bila mashabiki, wakati kuna baadhi ya timu zinaruhusiwa.

Alishindwa kujua kuwa Tanzania ni moja kati ya nchi za Afrika ambazo hazijaathiriwa kwa kiasi kikubwa na ugonjwa wa COVID-19 unaosababishwa na virusi vya corona, huku wananchi wake wakielekezwa kuchukua hatua kadhaa na wakitekeleza, lakini serikali ikiwataka kuendelea na maisha yao ya kawaida waliyoyazoea.

Sitaki kwenda sana huko kwa sababu tayari CAF imeshakataza. Simba itakuwa ndani ya Uwanja wa Benjamin Mkapa na maofisa tu wa klabu yao, viongozi na watu wa karibu na si mashabiki.

Wachezaji wa Simba pamoja na kwamba wamecheza mechi kadhaa ugenini bila mashabiki na wamepata matokeo yote matatu ya mpira wa miguu, lakini hawajazoea kucheza nyumbani bila mashabiki. Nini kifanyike? Ni wakati sasa wanachama na mashabiki wa Simba kufanya njia mbadala itakayowafanya waangaliwe kwa jicho la tatu kuwa ni moja ya mashabiki bora kabisa nchini Afrika wanaoipenda timu yao.

Bila kuushirikisha uongozi mkuu wa Simba. Wanachama na mashabiki kupitia matawi yao, waombe Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam. Wafunge 'skrini' kubwa ya TV kwa ajili ya kuuangalia mpira huo. Wanachama na mashabiki wajae kwenye uwanja huo ambao upo karibu kabisa na ule wa Benjamin Mkapa huku taratibu zote za kiafya zikifanyika wakati wa kuingia.

Wengine pia wajazane nje ya Uwanja wa Benjamin Mkapa ambako pembeni huwa na baa na grosari. Huko kuwe na televisheni kubwa kwa ajili ya mashabiki kuangalia mpira.

Wajazane na ngoma zao kwa ajili ya kuwachanganya wapinzani, pamoja na kuwaonyesha wachezaji wa Simba kuwa pamoja na kwamba ndani wapo peke yao, lakini nje ya uwanja wapo pamoja na mashabiki ambao wamekuja kuwasapoti.

Kifupi ni kwamba mashabiki wa Simba wasikubali kuacha timu yao na upweke. wasikae majumbani. Watoke kama vile wanakwenda kuingia uwanjani, lakini waishie nje na Uwanja wa Uhuru.

Wachezaji wa Simba wakiona watu wamejazana Uhuru na wengine nje ya uwanja wakiwashangilia kwa nguvu, morali utakuwa juu zaidi. Sauti za kushangilia zitakazokuwa zinatoka Uhuru nazo zitakuwa ni kichocheo kwao.

Kwa wapinzani ambao tayari akili zao zinajua kuwa wanakwenda kucheza bila mashabiki, wakikuta umati wa mashabiki upo nje ya uwanja ukishangilia kwa nguvu, pia kelele za Uwanja wa Uhuru, zitawaathiri kisaikolojia na kuona hakuna tofauti yoyote ya kucheza bila mashabiki au mashabiki wakiwa uwanjani.

HABARI KITAIFA

# Zaidi ya watumishi 400 Muhimbili wapima figo

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuadhimisha Siku ya Figo Duniani ambayo hufanyika Machi 11, kila mwaka, watumishi zaidi ya 460 wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, wamepima kubaini kama wana magonjwa ya figo.

Akizungumza kuhusu upamaji afya kwa watumishi wa Muhimbili, Dk. Onesmo Kisanga, alisema hatua hiyo itasaidia watumishi kuanza mapema huduma za matibabu endapo uchunguzi utabainisha kama wana magonjwa ya figo.

"Tunapenda kuwapima afya watumishi wetu ili kama wana magonjwa ya figo, waweze kutibiwa mapema na kuendelea na shughuli za ujenzi wa taifa," alisema Dk. Kisanga.

Alisema upamaji wa afya kwa watumishi unahusisha, kupima kisukari, shinikizo la damu, uzito, mkojo pamoja na kutoa elimu ya afya.

"Watu wengi hawajui kama uzito unasababisha kisukari na shinikizo la damu sasa ili kuwa katika afya nzuri, tunapaswa kuwa makini na afya zetu kwa sababu uchunguzi unasaidia kuzuia uharibifu wa figo," alisema.

Alisema faida kubwa ya kupima afya mara kwa mara, inasaidia watu kupatiwa matibabu mapema endapo itabainika mtu au watu wana magonjwa ya figo.

# Wenye ulemavu watakiwa kubadili fikra

**Na Jenifer Gilla**

WANAWAKE wenye ulemavu wanapaswa kubadilisha fikra kutoka kuwa wapigakura wa wakati huo na kuwa wagombea katika nafasi za uongozi.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Ummy Nderiananga, katika Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliandaliwa na Shirika la Her Ability kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Wenye Ulemavu SHIWAVYATA kwa msaada wa Taasisi ya Foundation for Civil Society (FCS) Alhamisi.

Alisisitiza kuwa suala la kujumuishwa kwa wanawake wenye ulemavu katika uongozi ni la msingi, na kuyasihi washirika wa maendeleo na wadau wa ulemavu kuwekeza katika kuwajengea uwezo wanawake wenye ulemavu ili kuongeza umahiri wao.

"Wanawake wanapaswa kujua kwamba katika kukamilisha uongozi, kamati ya kuteua au wapigakura hufanya uamuzi kulingana na uwezo na umahiri, hivyo mnapaswa kuongeza kujistahi na kujiandaa kugombea nafasi za uongozi," alisema Naibu Waziri Ummy.

Pia aliwakumbusha wanawake hao kutumia mpango wa serikali wa asilimia 2 ya fedha kama fursa ya kujiimarisha kwa kuomba mikopo ili kujiinua kiuchumi.

Alisema katika kuwajali na kuwathamini watu wenye ulemavu, serikali imetenga asilimia mbili ya fedha za halmashauri kuwapatia mikopo watu wenye ulemavu.

Maadhimisho hayo ambayo yaliongozwa na kaulimbiu 'Ushiriki wa Wanawake Walemavu katika Uongozi Katika Mashirika ya Watu Wenye Ulemavu' yalihudhuriwa na wanawake wenye ulemavu kutoka sehemu mbalimbali nchini pamoja na wadau wa kundi hilo nchini.

Naye Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake Wenye Ulemavu Zanzibar, Salma Sadat, alisema moja ya mambo waliyoyapigania na kufanikiwa ni wanawake wenye ulemavu kusimamia asilimia 50 ya mashirika ya walemavu Zanzibar.

Alisema katika mashirika hayo wanawake wote walioshinda walichaguliwa kidemokrasia kupitia mchakato wa uchaguzi wenye ushindani.

Naye makamu Mwenyekiti wa SHIVYAWATA Mkoa wa Mbeya, Willam Simwali, alisema wanawake ambao wapo katika nafasi za uongozi waoneshe uongozi wa mabadiliko kwa kuonesha tabia zote muhimu kwa kiongozi kama vile kuunda njia ya kuwawezesha wengine na kuhamasisha maono ya pamoja ili kufikia malengo ya uongozi kwa wanawake.

Victoria Lihiru,Mhadhiri wa Chuo Kikuu Huria, ambaye alikuwa mtoa mada katika shughuli, alisema lengo la kupigania usawa wa uwakilishi wa watu wenye ulemavu si kuiba nafasi za wanaume bali kuleta usawa wa wakilishi wa matatizo kwa kuwa kuna baadhi ya matatizo yanatofautiana kati ya mwanamke na mwanamume.



Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, akiwahutubia wakazi wa kijiji cha Makomero, jana, alipokuwa akitafutia ufumbuzi wa kudumu mgogoro wa wafugaji na wakulima waliokuwa wakitumia Bonde la Serikali la Wembere wilayani Igunga. **PICHA: TIGANYA VINCENT**

# Wawekezaji wa chai walia na miundombinu

**Na Mwandishi Wetu,** NJOMBE

WAWEKEZAJI wa chai nchini wameiomba serikali kupitia Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) kufanya maboresho ya miundombinu ya barabara ili kurahisisha usafirishaji wa majani mabichi ya chai kufika viwanda kwa ajili ya kuchakatwa.

Meneja Mkuu wa kiwanda cha chai cha Kibena kinachomilikiwa na Kampuni ya DL Group Company Ltd, Mohamed Kasila, amesema ubovu wa barabara pamoja na umeme umekuwa ni kikwazo kikubwa kinachowaongezea gharama za uzalishaji wa zao la chai.

"Tunaiomba serikali ijenge miundombinu ili kufanya urahisi wa usafirishaji wa chai na hata pembejeo jambo hili litasaidia kuinua sekta ya chai katika uzalishaji wake na kipato kwa ujumla," alisema Kasila.

Alisema barabara nyingi zinazoingia katika mashamba zipo katika hali mbaya, jambo linalochangia uzalishaji wa chai kushuka kadhalika na wakulima kushindwa kufikia soko la zao lao kwa wakati na kusababisha kuharibika kutokana na miundombinu.

"Zao hili linapotolewa shambani linahitajika kufika kwa haraka kiwanda tayari kwa kuchakatwa hivyo linapochelewa kwa sababu ya miundombinu kuharibika kabla ya kufika kiwandani hivyo kusababisha hasara kwa mkulima," alisema Kasila. Aliongea faida ya zao hili kwa mkulima inapatikana pale majani yanapofika kwa wakati kiwanda kinyume na hapo husababisha hasara kwa mkulima na hata serikali kukosa mapato makubwa kwa sababu ya kiwanda kupokea malighafi chache kulinganisha na uwezo wa kiwanda chenyewe.

"Miundombinu ikiboreshwa hususani barabara hali ya uzalishaji itaongezeka na kupelekea wakulima kunufaika kupitia kilimo na serikali kuongeza pato kupitia kodi katika sekta hii ya chai," alisema Kasila.

Aidha, Kasila alisema kampuni inaendelea na zoezi la kuwalipa wakulima malipo yao yote ili kuendeleza ushirikiano ulipo kati ya wakulima na kiwanda pamoja na jamii inayokizunguka kiwanda.

"Lengo letu ni kuendeleza ushirikiano kati ya kiwanda na wakulima kwani sote tunategemeana katika kujenga mnyororo wa thamani wa zao la chai nchini, alisema Kasila.

Ofisa wa Kilimo wa TADB Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Ashura Akimu, alisema TADB imejipanga vizuri kuhakikisha inafanya uwezeshaji kwa wakulima wa zao la chai ili kuzalisha malighafi za kutoka zinazohitajika zao viwanda.

"TADB imesema wanatoa mikopo ya matrekta pamoja na mashine za usindikaji wa zao la chai kwa wakulima ili kukuza sekta iweze kuchangia pakubwa katika pato la Taifa," alisema.

Hivi karibuni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alifanya ziara mkoani Njombe na kukutana na wadau wa sekta ya chai na kutumia fursa hiyo kuwahakikishia wakulima kuwa serikali itawahimiza wawekezaji kulipa madai yote kwa wakati na watakuwa bega kwa bega na wakulima kuhakikisha tija ya uzalishaji wa zao la chai inaongezeka ili kumletea mkulima maendeleo.

# Wabunge waagiza ujenzi chumba cha kujifungulia

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

KAMATI ya Kudumu ya Bunge Utawala na Serikali za Mitaa imeiagiza serikali kupitia mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kujenga jengo la kujifungulia wajawazito na chumba cha maabara katika zahanati ya Kata ya Mkambarani katika wilaya ya Morogoro.

Agizo hilo lilitolewa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Humphrey Polepole, alipotembea miradi mbalimbali ikiwamo zahanati hiyo ambayo imejengwa kwa ufadhili wa TASAF.

Alisema licha ya ujenzi huo wa zahanati, lakini kamati imeona kuna umuhimu wa kuongeza chumba kingine cha kinamama kujifungulia.

"TASAF mmefanya kazi kubwa kwa ujenzi huu wa zahanati, lakini tunaiagiza serikali kuongeza chumba kingine cha kujifungulia, kilichopo hakitoshi kutokana na ongezeko la idadi ya watu," alisema Polepole.

Hata hivyo, alisema kazi kubwa iliyofanywa na serikali kupitia mfuko huo imeweza kuleta ukombozi mkubwa kwa wananchi wa Kata ya Mkambarani ambao walikuwa wakilazimika kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya.

Aliwataka wananchi hao kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) ili kupata matibabu ya uhakika kwani mfuko huo kwa sasa umeboreshwa na kutoa huduma bora za afya.

"Nimepata taarifa hapa Mkambarani wapo watu 26 tu ndio waliojiunga na CHF tunataka kila mwananchi ajiunge ili kuweza kupata huduma bora za afya," alisema Polepole.

Kwa upande wake Naibu Waziri Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora), Deogratius, Ndejembi, alisema serikali itatekeleza maagizo yote yaliyotolewa na Kamati hiyo ya Bunge ikiwamo kujenga chumba cha kujifungulia kinamama pamoja na ujenzi wa maabara.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha inatoa huduma bora za afya kwa wananchi wake ili kuondokana na maradhi ili waweze kufanya shughuli za kujiletea maendeleo.

TASAF katika Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro imetekeleza jumla ya miradi 19 kwa awamu ya kwanza ikiwa pamoja na mradi wa zahanati ya Mkambarani wenye thamani ya Sh. milioni 34.8.




Mkuu wa Wilaya ya Geita, Fadhili Juma (katikati), akiwa na Meneja wa Ulinzi kutoka GGML, George Kaijunga (kulia) na Meneja wa masuala ya kijamii- GGML, Joseph Mangilima, baada ya uzinduzi wa mfumo wa taarifa za ulinzi na usalama. **MPIGAPICHA WETU**

# GGML yazindua mfumo rahisi taarifa za usalama

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA jitihada za kushirikiana zaidi na jamii inayouzunguka mgodi, Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML), imezindua rasmi mfumo wa kutoa taarifa mbalimbali za ulinzi, usalama na za kijamii ambapo raia wema wamepatiwa fursa ya kupiga simu bure bila malipo.

Katika mfumo huo wa kidigitali, raia wema wanaozunguka eneo la mgodi wataweza kupiga simu namba 0800 750 145 bila malipo wanapobaini vitendo vya uhalifu vikiwamo kula njama, uharibifu wa mali za kampuni, vitendo vya rushwa kutoka kwa baadhi ya wafanyakazi au makandarasi wanaofanya kazi na kampuni ya GGML, vitendo vya kiusalama ikiwamo uendeshaji wa magari usio salama, na taarifa nyinginezo zote zinazoihusu kampuni.

Akizindua mfumo huo mkoani Geita, Mkuu wa Wilaya ya Geita, Fadhili Juma, alisema teknolojia ya habari na mawasiliano ni muhimu katika kipindi hiki ili kujibu changamoto mbalimbali zinazoikabili jamii ikiwamo uhalifu na hujuma ya miundombinu mbalimbali ikiwamo umeme au mabomba ya maji ambayo huigharimu serikali fedha nyingi.

"Naipongeza sana GGML kwa kuja na ubunifu huu kwa kuwa lengo lake litaisaidia pia serikali kupata taarifa mbalimbali za kiuhalifu.

Jukumu la serikali ni kuweka mazingira bora ya kumlinda mwekezaji ili afanye shughuli zake kwa usalama na ufanisi, akitoa ajira na kuchangia pato la taifa kupitia kodi na tozo mbalimbali," alisema.

Meneja Mwandamizi anayeshughulikia masuala ya ulinzi kutoka wa GGML, Suleiman Machira, alisema mfumo huo umekuja kipindi muafaka wakati kampuni ya GGML na wakazi wanaouzunguka mgodi huo wakiwa wameimarisha uhusiano mwema wa kindugu na kufanya shughuli zao kwa ushirikiano mkubwa.

"Tumekuwa na raia wema ambao wamekuwa tayari kutoa taarifa mbalimbali ambazo zingeisaidia kampuni,lakini wanashindwa kutoa taarifa kwa sababu ya kukosekana kwa mfumo rahisi usio na gharama wa kutoa taarifa," alisema Machira.

Machira aliongeza kuwa mwekezaji anapofanya shughuli zake kwa usalama bila kuhujumiwa au kufanyiwa vitendo vya kihalifu maana yake ataweza kufanya shughuli zake za uwekezaji kwa amani na kuchangia pato la uchumi wa mkoa wa Geita na Tanzania kwa ujumla.

# Wataja vyanzo ukiukwaji haki za watoto

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

MIGOGORO ya kifamilia, ndoa za utotoni na mimba zisizotarajiwa katika kata ya Mwakitolyo, Halmashauri ya Shinyanga Vijijini, mkoani Shinyanga, inachangia ukiukwaji wa haki za watoto na kuwasababishia kukosa masomo.

Pia sababu hizo zimetajwa kuwa ni miongoni mwa chanzo cha kutokea kwa vifo vitokanavyo na uzazi, maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi(VVU), ikiwamo saratani ya mlango wa shingo ya uzazi kwa watoto chini ya umri wa miaka 18.

Veronica Sostenes, mkazi wa kata hiyo, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na gazeti hili, kuhusu utekelezaji wa mradi wa nafasi ya vyombo vya habari katika kumaliza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto unaotekelezwa na SPC kwa ufadhili wa Women Fund Tanzania (WFT).

Alisema vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto vinaendelea kushamiri katika kata hiyo na kusababisha baadhi ya watoto hasa wa kike kuendelea kukosa masomo.

Naye Godfrey Bahati, alisema bado jamii zinaendelea kukumbatia mila na tamaduni potofu ambazo zinachangia kuongezeka kwa matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto hali ambayo inasababisha kumkwamisha mwanamke kutimiza ndoto zake katika suala la elimu na kiuchumi.

"Vijijini bado kuna wazee wenye umri mkubwa wanaoa watoto chini ya umri wa miaka 18, huku baadhi ya wazazi wakitajwa kushiriki kuozesha wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kwa ajili ya kupatiwa fedha ama mifugo bila ya kujua athari zinazoweza kuwapata wanapoolewa," alisema Bahati.

Alisema ndoa hizo zinaweza kuwa kichocheo cha watoto kupata maambukizi ya magonjwa ya ngono kutokana na wengi wao kutokuwa na uelewa ya elimu ya afya ya uzazi na kwamba ili kutatua suala hilo wahusika wachukuliwe hatua za kisheria.

Kwa upande wake mkazi wa eneo hilo, Sikitu Nigo, alisema wanaopiga ramli chonganishi vijijini wanawashawishi wanaume kufanya mapenzi na watoto wenye umri mdogo kwa lengo la kupata mali hali ambayo inasababisha ongezeko la mimba za utotoni.

Ofisa Maendeleo ya Jamii katika kata ya Mwakitolyo, Mussa Gongo, alisema anashirikiana na wenyeviti wa serikali za mitaa na kamati za mtaa kutokomeza vitendo vya kikatili kwa wanawake na watoto na kuhakikisha watoto wenye umri wa kwenda shule wanasoma.

Gongo aliwataka wazazi na walezi kupiga vita vitendo vya ukatili dhidi ya watoto na wanawake ili kuhakikisha wanapata haki zao za msingi ikiwamo elimu na kutengeneza taifa lenye wasomi.

Aliongeza kuwa katika kufikia usawa wa asilimia 50 kwa 50, jamii inapaswa kubadilika na kuacha mfumo dume na mila kandamizi dhidi ya wanawake na watoto ili kutoa fursa ya kupata haki sawa katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo na kumiliki mali.

## Mkakati waanza kukabili ushindani soko kimataifa

**Na Elizabeth Zaya**

TANZANIA imezindua umoja wa wadau wa Ubora ambao utatumika kama jukwaa la kusaidia wazalishaji wa bidhaa na watoa huduma kuzalisha na kutoa huduma za kiushindani katika soko la kimataifa.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa umoja huo jijini Dar es Salaam, mratibu wa mradi wa kusaidia wajasiriamali Tanzania katika kuongeza thamani kwenye bidhaa na huduma(MARKUP), Safari Fungo, alisema hatua hiyo imeweka historia na itasaidia kuchagiza katika kukuza zaidi uchumi wa nchi.

Alisema wazalishaji wengi wa bidhaa na watoa huduma, wamekuwa wakipata changamoto kubwa kwenye ushindani katika soko la kimataifa kutokana na kukosekana kwa jukwaa la kujadili namna ya kutatua matatizo yaliyopo katika sekta hiyo na kuyatafutia ufumbuzi.

"Tumezindua Umoja wa Wadau wa Ubora nchini ikiwa ni matokeo ya mradi wetu, tunafahamu kwamba ubora upo kwenye huduma, bidhaa na kwenye kila kitu, kwa hiyo kupitia umoja huu utakuwa unakutanisha wadau kutoka katika sekta mbalimbali kuzungumzia fursa, changamoto na kupashana habari za maendeleo katika sekta hiyo kwa ajili ya kushindana katika soko la kimataifa," alisema Fungo.

Mwenyekiti wa Umoja huo, Amily Hamza, alisema kupatikana kwa usajili wa umoja huo kutasaidia kupandisha zaidi uchumi wa nchi kwa sababu matatizo mengi yaliyopo kwa sasa yatakuwa yanapatiwa ufumbuzi kwa haraka zaidi.

Pia alisema litatoa fursa kwa viwanda vya ndani kupeleka bidhaa nje ya nchi, kushindana na kuzalisha kwa ubora zaidi.

# H/shauri yawapa wajasiriamali bil. 2.6/-

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga imetoa Sh. bilioni 2.6 kwa vikundi vya wajasiriamali vijana, kinamama na watu wenye ulemavu kwa ajili ya kuviinua kiuchumi na kukuza mitaji yao kwa kipindi cha mwaka 2015 mpaka sasa.

Anderson Msumba, Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, aliyabainisha hayo wakati akizungumza na vyombo vya habari alipokuwa akitoa ufafanuzi wa utaratibu mpya wa ukopeshaji kwa makundi maalum.

Aidha, alisema kwa mwaka 2020 halmashauri imeshatoa Sh. milioni 700 kwa wajasiriamali wanawake kama mikopo kwa ajili ya kuwaendeleza pamoja na kuhakikisha kuwa mitaji yao ya kibiashara inakua na kujitegemea.

Hata hivyo, Msumba alisema, kiwango cha chini cha mkopo ni Sh. milioni tano na, kwamba katika kikundi cha ufugaji wa ng'ombe wa maziwa Kata ya Nyasubi kimepewa Sh. milioni 70, na kuwa maziwa yanayopatikana wanauzwa katika kiwanda cha maziwa kilichopo Kagongwa.

Alisema wanakikundi wanaruhusiwa kukopa fedha hizo hadi mara tatu wanapokopa na kurejesha kwa wakati, na kwamba mbali na mikopo hiyo, wanatoa mikopo ya kilimo kwa vikundi vyenye uwezo wa kulima hekari tano na kuendelea na kata za Nyandekwa na Kinaga wameshanufaika na mikopo hiyo.

Ashura Hoja, Ofisa Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Kahama, alisema halmashauri imevifikisha mahakamani vikundi 66 vya ujasiriamali vijana na wanawake vilivyokopesha mikopo hiyo kwa kushinda kulipa Sh. milioni 68.3 kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014 mpaka hivi sasa.



Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kambarage iliyoko mkoani Njombe, Jane Ng'umbi (watano kulia), akipokea msaada wa mifuko ya saruji 100 kutoka kwa Kaimu Meneja Mwandamizi wa Uhusiano wa Benki ya TPB, Chichi Banda (watatu kushoto). Saruji hiyo itatumika kujenga madarasa 7 ya shule hiyo na ofisi ya walimu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mikoa mitano yapewa vifaa vya elimu, afya

**Na Mwandishi Wetu**

MIKOA mitano imepatiwa vifaa mbalimbali kwa lengo la kuboresha sekta ya elimu na afya.

Vifaa hivyo vimetolewa na Benki ya NMB kwenye halmashauri mbalimbali za mikoa ya Mara, Manyara, Singida, Ruvuma na Mtwara vikiwa na thamani ya zaidi ya shilingi milioni 70.

Vifaa vilivyotolewa ni meza, viti, madawati, mabati, mbao, misumari pamoja na vitanda kwa ajili shule za bweni, ambapo vifaa vyote vimetolea mwishoni mwa wiki hii vikiwa na lengo la kuboresha utolewaji ewa huduma katika sekta hizo.

Katika Halmashauri za Mji Mbulu na Mbulu Vijijini mkoani Manyara imetoa meza 50 na viti 50, kwa shule mbili za Sekondari Masiende pamoja na Gehandu vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 10.

Msaada huo umetajwa kuwa mkombozi mkubwa kwa wanafunzi waliochaguliwa kwenda Shule ya Sekondari Masienda kupunguziwa adha ya kutembea umbali wa zaidi ya kilometa 10 kwenda katika Shule ya Sekondari Gunyoda kutokana na shule hiyo kutokuanza rasmi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mbulu, Hudson Kamoga, alisema kuwa msaada huo utawapunguzia adha wanafunzi waliochaguliwa sekondari kutembea umbali wa zaidi ya kilometa 10 kwenda kufuata masomo Shule ya Sekondari Gunyoda iliyoko jirani.

Vifaa hivyo vilikabidhiwa na Meneja wa benki hiyo Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi, ambaye alieleza lengo la kutoa vifaa hivyo ni kuondoa adha ya wanafunzi kutembea umbali mrefu ambao waliochaguliwa kujiunga na shule hiyo.

Katika Mkoa wa Mara benki hiyo imetoa vifaa kwa ajili ya miundombinu ya elimu vyenye thamani ya Sh. milioni 11.5 kwa shule 2 za Halmashauri ya Wilaya na Mji wa Tarime.

Vifaa vilivyotolewa ni mabati, mbao na misumali kwa ajili ya kuezeka Shule ya Msingi Nyamwino iliyopo halmashauri ya mji wa Tarime iliyoezuliwa na upepo pamoja na madawati 50 kwa ajili ya Shule ya Msingi Nyamumbara iliyoko Halmashauri ya Wilaya ya Tarime.

Akikabidhi vifaa hivyo kwa Mkuu wa Wilaya ya Tarime, mhandisi Mtemi Msafiri, Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Ziwa, Baraka Laduslaus, alisema msaada huo ni sehemu ya kurudisha faida kwa jamii.

Msafiri, aliishukuru benki hiyo kwa msaada walioutoa na kuwataka wahusika kuanza mara kutumia vifaa hivyo kama ilivyokusudiwa.

Katika Wilaya ya Iramba Mkoani Singida, NMB imetoa madawati 100 kwa ajili ya shule ya msingi Kisiriri na Tyegelo, huku shule ya Sekondari Kisiriri ikipatiwa vitanda 50.

Akipokea vifaa hivyo Katibu tawala wa Wilaya hiyo, Pius Sangoma, aliwataka walimu kusimamia nidhamu ya utunzaji wa vifaa kwa wanafunzi vinavyotolewa na serikali pamoja na wadau wa maendeleo katika shule zao.

Meneja wa NMB Kanda ya Kati ,Nsolo Mlozi akikabidhi vifaa hivyo alisema kuwa vifaa vyote vina thamani ya shilingi Milioni 22.

Mkoani Mtwara Benki hiyo imetoa mabati 105 yenye thamani ya shilingi milioni tano katika hospitali ya Rufaa ya Ligula Mkoani Mtwra kwa ajili ya kusaidia kukarabati wodi ya watoto.

Mganga Mfawidhi wa hosptali hiyo, Dkt. Robikieki Kisambu, aliishukuru benki hiyo kwa msaada huku huku akieleza inakabiliwa na uchakavu wa miundombinu na haikidhi mahitaji kwa wagonjwa na watumishi.

Meneja wa Kanda ya Kusini Janeth Chango, a alisema msaada huo wa mabati ni sehemu ya jukumu la NMB katika kusaidia upatikanaji wa huduma bora za afya kwa jamii.

Katika Mkoa wa Ruvuma NMB imetoa msaada wa vifaa vyenye thamani ya shilingi milioni 12 katika shule tatu za msingi zilizopo Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma.

,Meneja wa benki hiyo Kanda ya Kusini, Janeth Shango, alizitaja shule zilizopata vifaa hivyo kuwa ni shule ya msingi Legele iliyopata mabati 60 kwa ajili ya kuezeka darasa la kwanza na choo.

Shule nyingine ni Mshanganokati iliyopewa madawati 80 na shule ya msingi Chandamali ambayo imepewa meza 21,viti 21 na kabati nne ambapo amesisitiza kuwa Benki ya NMB imeamua kushirikiana na jamii kwa kutoa msaada katika shule hizo tatu.

## HABARI KITAIFA




Wanafunzi, walimu na watumishi wa NMB wakifurahia msaada wa madawati 80 yaliyotolewa na Benki ya NMB kwa Shule ya Msingi Mshanganokati Manispaa ya Songea, shule hiyo inakabiliwa na upungufu wa madawati na kusababisha baadhi ya wanafunzi kukaa chini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TARURA yataka wanaoharibu miundombinu kukemewa

**Na Mwandishi Wetu,** MBINGA

MENEJA wa Mamlaka ya Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA), Halmashauri ya Mbinga Mji mkoani Ruvuma, Ismail Mafita, amewaomba madiwani wa halmashauri hiyo kuwakemea baadhi ya wananchi kwenye kata zao wanaofanya uharibifu wa miundombinu ya barabara kwa makusudi.

Mafita alitoa ombi hilo wakati akitoa taarifa ya utendaji kazi wa mamlaka hiyo pamoja na changamoto zake kwenye kikao cha Baraza maalum la Madiwani la Halmashauri ya Mbinga Mji lililokuwa likijadili na kupitisha rasimu ya bajeti ya mwaka 2021 na 2022 ya halmashauri hiyo na kupitisha bajeti ya Sh. bilioni 23.9.

Alisema mamlaka hiyo imekuwa ikijitahidi kuweka miundombinu ya barabara licha ya kuwapo kwa changamoto za ufinyu wa bajeti pamoja upungufu wa watumishi, hata hivyo, baadhi ya wananchi wamekuwa wakihujumu miundombinu.

Akifafanua kuhusu uharibifu huo, alisema katika kipindi cha mwaka 2019 na 2020 baadhi ya barabara ziliwekewa vibao visivyopungua 50 vya kuitambua mita pamoja na majina ya barabara hizo, lakini vimeondolewa na kubaki vitano pekee jambo ambalo linarudisha jitihada za maendeleo zinazofanywa na serikali.

"Ndugu zangu waheshimiwa madiwani kibaya zaidi wanaofanya uharibifu huo ni baadhi ya wananchi wenu mnaowaongoza kwenye kata zenu, mimi nawaombeni kupitia baraza hili mkatusaidie kuwaelimisha wananchi hao pamoja na kuwakemea wasifanye uharibifu huo," alisema Mafita.

Akizungumzia utendaji kazi wa mamlaka hiyo, alisema wameshatambua eneo la halmashauri hiyo lina kilomita 1063.51, zilizosajiliwa, barabara 502 na kila barabara itapewa jina la utambulisho mchakato unaoendelea utakapo kamilika.

Alisema hiyo itasaidia kila diwani kwenye kata yake kutambua barabara alizonazo kwa majina pamoja na kilomita zake ili kuwarahisishia katambua barabara zitakazokuwa kwenye mpango.

Kwa upande wake, Makamu Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, David Mapunda, aliiomba TARURA kujipanga kuweka taa za barabarani kwenye baadhi ya barabara ambazo zinatumiwa muda wote ikiwamo ya Hospitali ya Halmashauri ya Mbinga Mji (Mbuyula) ili watumiaji waweze kupita kwenye mwanga hasa wanapoenda kupatiwa huduma wakati wa usiku.

Naye Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Kelvin Mapunda, wakati akipokea ombi la Mafita, alisema suala hilo limechukuliwa na madiwani wanatakiwa kulitekeleza.

# Wanahabari wahamasishwa vita ukatili dhidi ya watoto

**Na Elizabeth Zaya**

MKURUGENZI wa Mfuko wa Kuwezesha Vyombo vya Habari Tanzania (TMF), Fausta Musokwa, amesema vyombo vya habari vina fursa kubwa ya kutumia nafasi yake katika kutoa mchango wake dhidi ya mapambano ya kukomesha ukatili kwa watoto.

Akizungumza wakati akifungua mafunzo ya siku mbili kwa waandishi wa habari za watoto kutoka mikoa mbalimbali nchini, yaliyofanyika Dar es Salaam, Mkurugenzi huyo wa TMF, alisema wanatambua kwamba vyombo hivyo vimetoa mchango wa kutosha katika vita hivyo dhidi ya ukatili kwa watoto, lakini bado kuna haja ya kuendeleza mapambano hayo mpaka kuhakikisha vinatokomezwa kabisa.

"Tunafahamu kwamba vyombo vya habari vimefanya kazi kubwa katika kuibua vitendo vya ukatili ambavyo vilikuwa vikifanywa kwa kificho katikati ya jamii yetu na tumeanza kuona impact yake, lakini bado havijaisha na katika ripoti mbalimbali ambazo zimekuwa zikitolewa, vitendo hivyo vinaendelea kufanyika katika nchi yetu, na ndiyo maana nina sema bado kama vyombo vya habari tuna wajibu wa kuendeleza mapambano ili kuhakikisha vinakomeshwa kabisa," alisema Musokwa.

"Kuwalinda watoto ni kazi yetu sisi sote, tunaweza kuwa na imani tofauti lakini ni jukumu ambalo tumepewa na Mungu kuwalinda na pasipo kufanya hivyo, hatuwezi kupata maendeleo katika jamii zetu wala katika nchi kwa sababu hao ndio tunawategemea kesho, viongozi tunaowaona sasa na watumishi katika sekta mbalimbali na hata wasio watumishi kila mmoja alipita katika hatua hii ya utoto, kwa hiyo tusiwapoteze viongozi wetu hawa wa kesho."

Alisema namna pekee ambayo itasaidia kufanikiwa katika vita hiyo ya kukomesha ukatili dhidi ya watoto hao ni kuibua taarifa za ukatili na kuzichambua kwa usahihi na kuziripoti mwanzo hadi mwisho pale wahusika wanapochukuliwa hatua za kisheria.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi inayojishughulisha na haki za Watoto (CRMF) Janeth Sosthenes, alisema wana imani kubwa na vyombo vya habari katika vita hiyo kwa kuwa yapo mambo mengi ambayo yamepatiwa ufumbuzi kutokana na kazi kubwa inayofanywa na vyombo hivyo vya habari.

Mwakilishi wa Shirika la kuwezesha taasisi za kutetea haki za watoto Tanzania(CRVPF), Eddah Durnken, alisema ipo haja kwa kila mtu katika nafasi yake kuanzia katika ngazi ya familia, jamii hadi serikali kuu, kushiriki katika vita hiyo ya kuwakomboa watoto dhidi ya vitendo vya ukatili.

# Miti yapandwa Kongwa kutunza mazingira

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL), imeungana na viongozi pamoja na wananchi wa wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma katika zoezi la upandaji miti ikiwa ni sehemu ya mpango wa kampuni hiyo wa kutunza mazingira.

Spika wa Bunge, Job Ndugai na viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa walikuwa ni baadhi ya viongozi walioshiriki katika zoezi hilo la upandaji miti lililofadhiliwa na SBL.

Akizungumza wakati wa zoezi hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti, alisema upandaji miti katika wilaya ya Kongwa ni sehemu ya mkakati endelevu wa kampuni hiyo unaolenga kupanda maelfu ya miti sehemu mbalimbali nchini.

Mkurugenzi huyo alisema mwaka 2019 kampuni hiyo ilipanda miti katika wilaya za Same na Moshi ili kuongeza uoto katika maeneo ya jirani na Mlima Kilimanjaro.

"SBL inachukulia miti kama sehemu muhimu sana ya mazingira. Miti inasaidia kuhifadhi vyanzo vya maji, ni makazi kwa wanyama na wadudu mbali mbali, inavuta hewa chafu ya kaboni na kuzalisha hewa safi na pia miti ni chanzo cha dawa. Biashara yetu na jamii kwa ujumla ni sehemu ya mazingira na hii itunafanya kuwa jukumu letu sote kuyalinda na kuyatunza mazingira," alisema Mark.

Upandaji miti wa SBL unakuja katika kipindi ambacho dunia inahangaika kupunguza uzalishaji ya hewa ukaa ili kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi pamoja na kuyalinda mazingira kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo

Kwa upande wake Spika Ndugai aliishukuru kampuni ya SBL kwa kuunga mkono jitihada za upandaji miti na kuongeza kuwa miti ina nafasi ya kipikee kwa maisha ya watu na kusistiza kuwa bila miti hakuna maisha.

Ndugai alisema ukataji miti holela ni moja kati ya sababu za mabadiliko ya tabianchi ambayo yamesababisha changamoto nyingi zinazomkabili binadamu ikiwa ni pamoja na athari kwenye uzalishaji wa chakula, upatikanaji wa maji, afya ya viumbe mbalimbali ikiwa ni pamoja na binadamu.

# Bil. 3.5/- kupeleka maji kwenye vijiji

**Na Jumbe Ismailly,** IGUNGA

WAKALA wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Igunga, mkoani Tabora, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2021/2122 unatarajia kutumia jumla ya shilingi 3,507,100,000 kwa ajili ya upanuzi wa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda katika vijiji kumi.

Kaimu Meneja wa RUWASA Wilaya ya Igunga, Harubu Maulidi, aliyasema hayo kwenye mkutano maalumu wa Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya wilaya hiyo uliolenga kupitisha rasimu ya mapendekezo ya mpango wa bajeti ya mwaka wa fedha wa 2021/2022.

Alivitaja vijiji vitakavyonuifa Mwabatima. Bukama, Mwamashimba, Kining'inila, Jogaya, Mwanyagula, Iyogewe, Isakamaliwa, Kidaru, Imalanguzi, Mwamakona na Ganyawa.

Alisema upanuzi wa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Kijiji cha Mwamashiga unatarajia kutumia Sh. 315,900,000.

Baadhi ya wajumbe wa mkutano huo waliushauri wakala huo kusitisha shughuli za utafiti walizopanga na badala yake fedha walizonazo zitumike katika kusambaza maji kwa wananchi.

Nipashe
Spotika



KOCHA GANI KUKAMILISHA 10 WALIOTEMWA LIGI KUU BARA? UK. 14



# SABABU 5 KWA NINI MESSI ATABAKI BARCA

**BARCELONA, Hispania**

LIONEL Messi bila shaka yoyote ni mmoja wa wachezaji bora zaidi wa wakati wote duniani. Lakini je, kipindi kinachokuja cha majira ya joto kinaweza kushuhudia nyota huyo wa Argentina akiondoka Barcelona?

Messi kuondoka Barcelona ni jambo linalowezekana, hasa ukichukulia ukweli kwamba, mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu. Lakini ataweza kubakia pale Camp Nou?

Kuna uwezekano mkubwa Messi akaamua kubaki Barcelona na hapa tunaangalia sababu tano za kwa nini atabaki hapo, twende sasa...

**#1. Rais mpya Joan Laporta**

Bila shaka yoyote Barcelona haijawa na mwenendo mzuri katika misimu ya hivi karibuni.

Miamba hao wa Catalunya wanalisaka taji la Ligi Kuu, LaLiga, na sasa wapo nafasi ya pili kwenye msimamo. Lakini wameshatolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na Paris St. Germain hatua ya 16-bora.

Wiki iliyopita klabu hiyo ilipata rais mpya baada ya kujiuzulu kwa Josep Maria Bartomeu Oktoba mwaka jana. Joan Laporta amerudi kuiongoza klabu hiyo ambayo aliwahi kuwa rais wake kati ya mwaka 2003 na 2010.

Kipindi ambacho Barcelona ilikuwa na mafanikio makubwa zaidi kwenye soka na Laporta ameshaweka wazi kwamba, anataka kumbakiza Messi hapo Nou Camp.

Rais huyo alinukuliwa akisema, "mchezaji bora duniani anaipenda Barca, na nina matumaini atasaini mkataba mpya wa kubakia Barcelona, kitu ambacho wote tunakitaka."

Laporta na Messi wana uhusiano wa karibu kwa kipindi kirefu, na hivyo ana nafasi kubwa ya kumshawishi kubaki hapo.

**#2. Klabu kushindwa kumnunua Messi**

Kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, dunia ya soka imekumbwa na kuanguka kwa uchumi na hivyo, klabu nyingi hazitaweza kumnunua Messi.

Kwa mujibu wa mkataba wa sasa wa Messi, analipwa pauni 500,000 kwa wiki, akiwa ndiye mchezaji anayelipwa kiasi kikubwa zaidi cha fedha duniani.

Hivyo kwa namna yoyote kama Messi ataondoka Barcelona kipindi cha majira ya joo klabu itakayomchukua italazimika kumlipa mshahara mkubwa zaidi, kitu ambacho kinaonekana kuwa kigumu.

**#3. Staili ya uchezaji**

Staili za klabu nyingi za uchezaji kwa sasa haziwezi kumfiti Messi, kwani timu zimekuwa zikicheza soka la kushambulia kwa kasi.

Pamoja na yote Messi sasa umri unamtupa mkono, hivyo staili ya soka la kasi kwa timu nyingi zinavyocheza kama Manchester City, Bayern Munich na Liverpool haiwezi kumfiti Messi.

Messi ambaye sasa ana umri wa miaka 33, kasi yake dimbani imepungua, hivyo hataweza kuendana na kasi ya staili ya kushambulia kwa kasi.

**#4. Kuirudisha Barca juu**

Kwa sasa Barcelona inalisaka taji la Ligi Kuu Hispania, LaLiga na utawala wake kwenye soka la Ulaya umemalizika.

Miamba hao wa Catalunya kwa mara ya mwisho kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya ilikuwa ni msimu wa 2014-15.

Kuna sababu nyingi kwa hili. Aina ya wachezaji ambao waliipa mafanikio makubwa Barcelona kwa kipindi cha muongo mmoja uliopita wamestaafu au wameondoka hapo Nou Camp.

Ni Messi pekee ndiye amebaki na anapambana kutaka kuirudisha klabu hiyo juu. Usajili wao wa hivi karibuni wa wachezaji kama Philippe Coutinho, Ousmane Dembele na Antoine Griezmann - unaonekana kushindwa kufanya kazi.

Lakini jambo moja ambalo Messi analitaka kwa sasa ni kuifanya klabu hiyo kurudi tena juu.

Na itarudi vipi? Kwa Messi kuendelea kuwa na wachezaji makinda wanaochipukia na wenye vipaji vya ukweli kama Pedri, Francisco Trincao na Ansu Fati.

Kama Messi akiweza kuirudisha tena Barca juu, maana yake kwamba atabaki kutambulika kama gwiji wa wakati wote wa Barcelona.

**#5. Familia yake**

Kama Messi atataka kuondoka Barcelona, klabu yake tangu utotoni, litakuwa chaguo lake mwenyewe.

Messi hatumii muda wake kwenda kwenye mji wa nyumbani kwao Argentina, Rosario, ambako ndugu zake wengine wanaishi huko. Lakini muda wake wote anaishi Barcelona pamoja na mke wake, Antonella Roccuzzo na watoto wao watatu.

Na familia ya Messi inaishi kwenye jumba la kifahari na maisha ya kifahari sana kule Castelldefels.

Jumba lake lina uwanja wa mpira, gym, mabwawa ya kuogelea na lipo pembeni mwa bahari ya Balearic.

Na kwa mujibu wa ripoti eneo ilipo nyumbani yake ni sehemu ambayo ndege haziruhusiwi kupita juu kwa mujibu wa sheria zilizowekwa na mamlaka ya Catalunya.


Hivyo, kwa namna yoyote, familia yake haitakuwa tayari kuondoka eneo kama hilo na kwenda kuishi kwingine.

Anaweza kuondoka na kwenda kujiunga na klabu nyingine, lakini kwa namna yoyote familia yake itabaki Barcelona.

Lakini kutokana na sheria za usafiri kwa sasa kuwa ngumu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, hilo litampa wakati mgumu Messi kusafiri mara kwa mara kurudi Barcelona. Na ni wazi kwamba, Messi hatakuwa tayari kuondoka na familia yake, hivyo kuna uwezekano mkubwa wa kubakia klabuni hapo.

## ISIKUPITE

ROBERT Lewandowski amefikia rekodi ya mfungaji wa pili wa wakati wote kwenye Bundesliga baada ya juzi kufunga wakati Bayern Munich ikishinda 3-1 dhidi ya Werder Bremen, hivyo bao hilo linamfanya kuifikia rekodi ya Klaus Fischer ya mabao 268 katika ligi hiyo, ni Gerd Muller pekee aliye juu yao, akiwa na mabao 365.



Extra Time

# NYOTA KUMI WA LIGUE 1 WANAOWEZA KUHAMIA EPL



DEPAY

**LONDON, England**

MOJA ya ligi kubwa tano za Ulaya ni Ufaransa, Ligue 1, ambayo ina wachezaji wengi wenye vipaji vya ukweli. Hata hivyo, katika miezi ya hivi karibuni imefunikwa na kivuli cha matatizo ya kifedha, kilichosababishwa na kuanguka kwa haki ya matangazo ya televisheni, ambayo yalikuwa na thamani ya kama euro bilioni 3.25.

Kutokana na mdororo huo wa uchumi, Ligue 1, inaweza kushuhudia nyota wake wengi wakihamia kwenye Ligi Kuu England kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

Na tayari mwanzo wake umeanza kuonekana, kwani kiungo mwenye kipaji cha ukweli, Morgan Sanson alijiunga na Aston Villa wakati wa dirisha la Januari akitokea Marseille kwa dili la uhamisho wa pauni milioni 14.

Ingawa matajiri, Paris St. Germain wanaweza wasiuze wachezaji wao, lakini hilo litakuwa tofauti kwa klabu nyingine za Ligue 1.

Kwa maana hiyo, hapa tunaangalia nyota 10 wanaotamba Ligue 1 ambao wanaweza kuhamia kwenye Ligi Kuu England, hawa hapa...

**#1. Jason Denayer (Lyon)**

Mlinzi wa Lyon, Jason Denayer amejiimarisha kama mmoja wa mabeki bora kwenye Ligue 1. Kama ilivyo idadi ya wachezaji kwenye orodha hii, Denayer tayari alishacheza kwa muda mfupi kwenye Ligi Kuu England.

Kinda huyu wa kimataifa wa Ubelgiji alitumia miaka kadhaa akiwa kwenye akademi ya Manchester City.

Lakini alipopelekwa kwa mkopo Celtic, Galatasaray na Sunderland hakuwa tena na nafasi pale kwenye dimba la Etihad na akauzwa Lyon kipindi cha majira ya joto mwaka 2018 kwa euro milioni 6.5.

Tangu hapo Denayer amejiimarisha yeye mwenyewe na kupata nafasi ya kuwa kikosi cha kwanza cha timu ya Taifa ya Ubelgiji na bila shaka yoyote ni mmoja wa walinzi bora wa kati kwenye Ligue 1.

**#2. Renato Sanches (Lille)**

Ni mmoja wa viungo bora kabisa, na Renato Sanches alibeba Kombe la Mataifa ya Ulaya, Euro 2016, akiwa na kikosi cha Ureno.

Sanches alisajiliwa kwa fedha nyingi kutoka Benfica kwenda Bayern Munich kwa euro milioni 35, lakini usajili huo haukuwa na manufaa kwake.

Baada ya kuwa na wakati mgumu kwa misimu minne kule Bayern - akahamia Ligi Kuu England katika Klabu ya Swansea City.

Hata hivyo, kipindi cha majira ya joto cha mwaka 2019 alihamia Lille na msimu wake wa kwanza kwenye Ligi Kuu Ufaransa ulikuwa na mafanikio, kwani alicheza mechi 19 akifunga mabao matatu na kutoa pasi moja ya mwisho.

Sanches sasa anaonekana kurudi kwenye ubora wake kama iliyvokuwa wakati wa michuano ya Euro 2016.

Anaonekana kuwaniwa na Liverpool na anatajwa kwamba anaweza kwenda kuwa mrithi wa Gini Wijnaldum ambaye anataka kuondoka.

**#3. Gael Kakuta (Lens)**

Safari ya Gael Kakuta, ambaye kwa sasa anacheza pale Lens ni ya kufurahisha kidogo. Mwanzo alisajiliwa katika akademi ya Chelsea akiwa na umri wa miaka 17, na akaondoka kwa 'Blues' hao mwaka 2015.

Kakuta akaenda kucheza Hispania na China kabla ya kurudi Ufaransa kipindi cha majira ya joto mwaka 2019. Uhamisho wake wa kwenda Amiens hakufanya kazi vizuri kwani timu hiyo ilishuka daraja.

Hata hivyo, tangu ahamie Lens kwa mkopo kipindi cha majira ya joto mwaka 2020, Kakuta haraka amekuwa mmoja wa wachezaji wenye kiwango bora kabisa.

Amecheza mechi 23 kwenye Ligue 1 pale Lens msimu huu, akifunga mabao tisa na kutoa pasi za mwisho nne.

Katika umri wake wa miaka 29, Kakuta anaonekana wazi kwamba, ana nafasi ya kucheza tena Ligi Kuu England.

**#4. Eduardo Camavinga (Rennes)**

Ndio kwanza ana umri wa miaka 18 na Eduardo Camavinga amekuwa na kiwango cha kuvutia sana pale Rennes.

Mzaliwa huyu wa Angola tayari ameshaitwa kwenye timu ya taifa ya wakubwa ya Ufaransa, na kuvunja rekodi ya kuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kuichezea na kuifungia bao Les Bleus.

Amekuwa akihusishwa na kuwaniwa na Manchester United, na kuna uwezekano akatua kule kipindi cha majira ya joto.

**#5. Florian Thauvin (Marseille)**

Wiga huyu wa Marseille, Florian Thauvin kuna wakati alichukuliwa kama kichekesho kwenye Ligi Kuu England.

Wakati akiwa Newcastle United msimu wa 2015-16, alikuwa mtu mwenye vituko vingi kwa uvaaji wake, hadi mashabiki na wachambuzi kumchukulia kama mchezaji asiye na maadili.

Lakini Thauvin kwa sasa ni mmoja mastraika bora kabisa Ulaya tangu aliporudi Ufaransa katika Klabu ya Marseille mwaka 2016.

Katika msimu wake wa kwanza pale kwenye dimba la Velodrome alifunga mabao 15 na kutoa pasi za mwisho nane na msimu wa 2017-18 alifunga mabao 22 na kutoa pasi za mwisho 11.

Na msimu wa 2018-19 akahusika na mabao 20 kwenye ligi na kufanya ahusishwe na kurudi EPL. Msimu wa 2019-20 aliukosa wote kutokana na kusumbuliwa na majeraha pale Marseille. Lakini msimu huu amerudi na mabao saba na pasi za mwisho saba na kuna nafasi kubwa ya kurudi tena EPL.

**#6. Memphis Depay (Lyon)**

Mchezaji mwingine ambaye 'amefufukia' kwenye Ligue 1 baada ya kuwa na wakati mgumu kule Ligi Kuu England na sasa Memphis Depay anafanya vizuri pale Lyon.

Raia huyo wa Uholanzi alikuwa na wakati mgumu pale Manchester United, lakini kiwango chake cha sasa kimekuwa cha kuvutia zaidi.

Tangu ahamie Lyon, Depay amekuwa kwenye kiwango cha kuvuti zaidi, kwani msimu wa 2018-19 amefunga mabao 10 na pasi za mwisho 10. Na msimu wa 2019-20 alikumbwa na muda mwingi wa majeraha.

Msimu huu tayari amefunga mabao 13 na kutoa pasi za mwisho sita kwenye mechi 24.

Depay amekuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia Barcelona, lakini kwa sababu ya miamba hao wa Hispania wapo kwenye wakati mgumu wa kifedha, uhamisho huo unaweza usifanikiwe.

Badala yake ana nafasi ya kurudi kwenye Ligi Kuu England na pengine Man United wanaweza kumsajili tena.

**#7. Sven Botman (Lille)**

Lille kwa sasa wapo kileleni mwa msimamo wa Ligue 1, na kiwango bora cha Botman kwenye safu ya ulinzi kimeifanya timu hiyo kuruhusu mabao 15 tu katika msimu wa 2020-21.

Alisajiliwa kipindi cha majira ya joto kilichopita kwa ada ya uhamisho ya euro milioni 9 akitokea Ajax, na nyota huyo mwenye umri wa miaka 21, amekuwa na mafanikio makubwa tangu kutua kwake Ligue 1.

Botman amecheza kila dakika katika mechi 24 za Lille za Ligi msimu huu na kuifanya timu hiyo kuwa moja ya yenye safu ya ulinzi bora zaidi.

Hivi karibuni Tottenham imekuwa timu ya kwanza kuhusishwa na mpango wa kuwania kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21.

**#8. Gaetan Laborde (Montpellier)**

Licha ya kwamba wapo nafasi ya katikati kwenye msimamo wa ligi, Montpellier mara zote imekuwa ikitajwa kama timu inayocheza soka la burudani zaidi kwenye Ligue 1.

Mmoja wa wachezaji aliyetoa mchango mkubwa ni straika, Gaetan Laborde. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 26, amekuwa na Montpellier tangu mwaka 2018, lakini msimu huu unaonekana kuwa bora zaidi kwake.

Laborde amecheza mechi zote 24 za Montpellier na amefunga mabao tisa na kutoa pasi za mwisho saba.

Na sasa klabu za Ligi Kuu England zimekuwa zikihusishwa sana, ambapo Wolves, West Ham United, na Newcastle United zimekuwa zikitajwa kuwania saini yake.

**#9. Fabien Centonze (Metz)**

Ligi Kuu England bila shaka yoyote ina walinzi bora zaidi wa kulia, huku wengi wao wakiwa watoto wa nyumbani, Waingereza. Hata hivyo, kuna klabu nyingi zinazohitaji kuimarisha safu hiyo.

Na klabu hizo zinaweza kumtupia jicho Fabien Centonze wa Metz. Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 25, tayari amekuwa akitajwa kwamba anataka kuondoka Ligue 1 katika klabu hiyo ya Metz aliyojiunga nayo msimu wa 2019-20.

Centonze amekuwa akihusishwa na klabu za Aston Villa na Tottenham.

**#10. Boulaye Dia (Reims)**

Ligue 1 ina idadi kubwa ya washambuliaji bora, wakiwamo nyota kama Kylian Mbappe na Neymar. Lakini wakati Mbappe akisimama kama kinara wa mabao kwenye Ligue 1, cha kushangaza jina la Boulaye Dia wa Reims haliko mbali naye.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 raia wa Senegal, alionyesha uwezo mkubwa wa kufunga wakati alipotikisa nyavu mara saba katika msimu wa 2019-20, lakini sasa ana mabao 12 kwa jina lake msimu huu.

Nguvu na kasi ya Dia imefanya kuwa na kiwango bora zaidi, huku akiwa na uwezo mkubwa wa umaliziaji.

Dia tayari alishahusishwa kuwaniwa na Arsenal na sajili za hivi karibuni zimekuwa zikimhusisha na West Ham.

Kama akiendelea na kasi hii ya kufunga bilashaka yoyote atakuwa na mafanikio makubwa huko mbeleni. Na hivyo, halitakuwa jambo la kushangaza kumuona akitua kwenye Ligi Kuu England msimu wa 2021-22.

## Nukuu

"Mchezaji bora duniani anaipenda Barca, na nina matumaini atasaini mkataba mpya wa kubakia Barcelona, kitu ambacho wote tunakitaka," **Rais mpya wa Barcelona, Joan Laporta, akizungumzia dhamira yake ya kumbakisha mshambuliaji wa timu hiyo, Lionel Messi.**



"Muda utasema, sina umri wa miaka 21 tena. Ilikuwa kipindi kile, mwili unabadilika kutokana na muda. Huweza kucheza kama ulivyokuwa kijana, kwa sasa mambo yamebadilika," **mshambuliaji wa Tottenham, Gareth Bale.**



"Siwezi kufikiria juu ya kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya, kwa namna yoyote lazima tupambane kumaliza kwenye nne bora (Ligi Kuu), maana hali kwetu kwa sasa ni ngumu mno, tukishindwa kufanya hivyo maana yake tutaendelea kuwa vibaya na vibaya zaidi," **Kocha Mkuu wa Liverpool, Jurgen Klopp.**



# KOCHA GANI KUKAMILISHA 10 WALIOTEMWA LIGI KUU BARA?

**Na Adam Fungamwango**

MAISHA yanaenda kasi sana. Kwenye soka la sasa kufukuzwa makocha limekuwa ni jambo la kawaida sana. Hata zile zinazoitwa au kujiita timu ndogo nazo zimekuwa zikitimua makocha pale zinapoona hazijafanya vizuri.

Dunia ya sasa ya soka, kocha hapewi muda wa miaka minne ama mitano, mpaka sasa kama ilivyokuwa kwa kina Alex Ferguson, hiyo ikitokana na dunia ya soka la sasa watu kunataka matokeo zaidi.

Ndiyo maana tunaona kwenye ligi mbalimbali Ulaya, Afrika makocha wanatimuliwa kila uchao. Hata kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, tumeona Kocha wa Al-Merreikh ya Sudan, Mserbia Miadrag Jesic, akitimuliwa baada ya kuhudumu kwa siku chache tu, akichukua nafasi ya Didier Gomes aliyejiunga na Simba. Kocha huyo alitimuliwa baada ya sare dhidi ya Simba.

Katika Ligi Kuu Tanzania Bara nako, Machi 7, mwaka huu, klabu ya Yanga ilitangaza kuachana na kocha wake, Mrundi Cedric Kaze, muda mfupi tu baada ya timu hiyo kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Polisi Tanzania katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Tangu kuanza kwa Ligi Kuu Bara, kuna baadhi ya makocha wa timu mbalimbali wameonyeshwa mlango wa kutokea. Wengine walianza na timu tangu mwanzo na wapo pia walioanzia kati. Kuna waliotimuliwa kutoka timu moja na kwenda nyingine.

Hawa ni baadhi ya makocha wa timu za Ligi Kuu Tanzania Bara walioonja joto ya jiwe mapema tu, lakini katika orodha hii, haipendezi kumtaja aliyekuwa Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck kwa sababu yeye aliomba mwenyewe kuondoka, twende sasa...



Cedric Kaze

**#1. Zlatco Krmpotic - Yanga**

Ni kocha aliyetimuliwa kazi mwanzoni mwa Oktoba mwaka jana, baada ya kuhudumu kwenye klabu ya Yanga kwa miezi mitatu tu.

Kisa cha kutimuliwa ni kwamba Yanga haikuwa inacheza soka la kuvutia. Hakuwa amefungwa mechi yoyote kwenye Ligi Kuu. Zlatco alijiunga na Yanga Julai mwaka jana kuchukua nafasi ya Mbelgiji Luc Eymael. Na hadi Mserbia huyo anaondoka Yanga ilikuwa inaongoza ligi.

**#2. Maka Mwalwisi - Ihefu FC**

Huyu ni kocha ambaye alipandisha Ihefu Ligi Kuu Tanzania Bara. Lakini baada ya kuona mambo hayaendi vizuri uongozi wa klabu hiyo ukamtimua. Ilikuwa ni mwanzoni mwa Oktoba mwaka jana alipotimuliwa kutokana na mwenendo mbaya wa timu na nafasi yake kuchukuliwa na kocha Zuberi Katwila.

**#3. Zuberi Katwila - Mtibwa Sugar**

Kwa sasa ni kocha wa Ihefu. Lakini kabla ya kuwa kocha wa timu hiyo, alionyeshwa mlango wa kutokea kistaarabu na kwa kuandika barua ya kujiuzulu kwa sababu ana heshima kubwa kwenye klabu hiyo aliyowahi kuichezea.

Mtibwa ambayo msimu huu haiko vizuri, ilisababisha katikati ya Oktoba mwaka jana kocha Katwila kutimuliwa.

**#4. Amri Said - Mbeya City**

Amri Said yeye alitimuliwa mwishoni mwa Oktoba mwaka jana baada ya timu yake kufanya vibaya na kushika nafasi ya mwisho kwenye msimamo wa ligi akiwa na timu ya Mbeya City. Kwa sasa Amri anaifundisha Mwadui FC ambayo nayo iko hoi mkiani.

**#5. Thiery Hitimana - Namungo**

Ni kocha raia wa Rwanda ambaye ameifanyia makubwa, kuiinua na kuipatia umaarufu mkubwa klabu ya Namungo FC. Ndiye aliyeifanya hadi kupata tiketi ya kushiriki Kombe la Shirikisho Afrika (CAF). Lakini timu ilianza kupoteza mechi nyingi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara. Hatimaye akaonyeshwa mlango wa kutokea na nafasi yake kuchukuliwa na Hemed Suleiman 'Morocco'.

**#6. Aristica Cioaba - Azam FC**

Kocha huyu raia wa Romania alitimuliwa baada ya Azam FC kufanya vibaya kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara. Timu hiyo ambayo ilishinda mechi saba mfululizo na kuongoza ligi, ilianza kuangusha pointi moja moja. Uongozi wa Azam ukaamua kumtimulia mwishoni mwa Novemba mwaka jana, na George Lwandamina akachukua nafasi yake.

**#7. Fulgance Novatus - Gwambina**

Klabu ya Gwambina iliachana rasmi na kocha wake, Fulgence Novatus kutokana na matokeo yasiyoridhisha ya timu hiyo mwanzoni kabisa mwa Januari. Na hii ni baada ya matokeo mabovu ya timu yao iliyokuwa ikiyapata.


**#8. Mecky Mexime - Kagera Sugar**

Baada ya kucheza mechi tano mfululizo mwaka 2021 bila kupata ushindi, kocha wa siku nyingi wa klabu hiyo, Mecky Maxime, alifunguliwa mlango wa kutokea na nafasi yake sasa imechukuliwa na aliyekuwa msaidizi wake, Peter Manyika.

**#9. Cedric Kaze - Yanga**

Kocha wa Yanga, Kaze akawa mmoja wa makocha ambao msimu huu wametimuliwa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara. Ligi bado haijaisha nas kinachotazamwa sasa ni kocha gani atakayekuwa wa 10 kutimuliwa kabla ya mtifuano huo kufikia ukingoni?

**JE, WAJUA?**



SERGIO Aguero amehitimisha mechi 13 alizocheza kwa dakika 641 akipiga mashuti 24 bila kuziona nyavu kwenye Ligi Kuu England akiichezea Man City, baada ya juzi kufungwa kwa mkwaju wa penalti dhidi ya Fulham, hilo likiwa bao lake la kwanza tangu Januari 2020 dhidi ya Sheffield United, siku 417 zilizopita.



# Mhagama aishauri TUPSE kubadili mfumo utendaji

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, amekitaka Chama cha Wafanyakazi cha Sekta ya Ulinzi Binafsi na Polisi Jamii (TUPSE), kubadili mfumo wa utendaji kazi wao ili kupunguza migogoro inayoyumbisha utendaji wa chama hicho.

Akifungua kikao kazi mwishoni mwa wiki jijini hapa, alisema ni lazima wahakikishe wanaunda chama upya, wakisimamie na kukilea ili kuleta tija inayokusudiwa.

"Nikiangalia kesi zilizopo Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) ni nyingi, kwa mfano mwaka 2017 kulikuwa na mashauri 754, mwaka 2018 mashauri 798, mwaka 2019 mashauri 1861, mwaka 2020 mashauri 1448 na mwaka 2021 mashauri 1,068, hizi ni kesi nyingi sana, maana ndio kwanza mwaka huu umeanza lakini tayari mashauri yamefikia 1,068," alisema.

Alitoa mfano Kampuni ya Night Support ambayo wafanyakazi wake wana madai ya zaidi ya shilingi bilioni tisa huku chama kikiwapo bila ya kufanya jitihada zozote kwa wafanyakazi hao kulipwa.

"Lazima chama hiki muwe daraja na nguzo imara, sasa badala ya kutatua changamoto hizi nyie mmetulia tu, jipambanueni mjue wajibu wenu.

"Kikao hiki cha leo ndio cha mwisho, kaeni wekeni mikakati na mwisimamie mkishindwa kitakachofuata ni kukifuta chama, kikao hiki leo ndio msamaha wangu wa mwisho."

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa TUPSE, Charles Basindile, alihimiza suala la ushirikiano baina ya waajiri na vyama vya wafanyakazi.

"Kwa bahati ushirikiano wa vyama vya wafanyakazi na mwajiri upo kisheria lakini mara nyingi vyama vyenyewe ndio vinaleta ugumu," alisema.



Diwani wa Kata ya Mnadani, Paul Bankiye, akizungumza na wakazi wa mtaa wa Ndachi baada ya kuahirisha mkutano uliokuwa ukimsubiri Mkurugenzi wa Jiji ambaye ameshindwa kuhudhuria kusikiliza kero za wananchi hao, ikiwamo ya upimaji na utoaji wa vibali vya ujenzi kwenye eneo hilo jana, jijini Dodoma. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Watoto wa kike 800,000 kupatiwa elimu, ujasiriamali

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SHIRIKA la ufadhili wa masomo kwa watoto wa kike wanaoishi katika mazingira magumu (CAMFED) kwa kushirikiana na serikali linatarajia kuwawezesha watoto wa kike zaidi ya 800,000 kuwapatia elimu, ujuzi na ujasiriamali.

Msaada huo utatolewa katika kipindi cha miaka mitano kuanzia 2021/2025.

Hayo yalisemwa jijini hapa na Mkurugenzi wa CAMFED, Lidya Wilbert, wakati akiwasilisha mpango mkakati wa Shirika hilo wa miaka mitano kwa ajili ya kuwawezesha watoto hao kiuchumi katika mambo mbalimbali.

Lidya alifafanua kuwa kati ya hao wanatarajia kuwapa wasichana wasomi 49,000 ambao watakuwa na uwezo wa kuwasaidia wengine, kila mmoja atawafadhili watoto 29.

"Tunafanya kazi ya kuwawezesha watoto hawa kupata mahitaji muhimu ya kielimu ili wawe wanahudhuria shuleni, lakini hatukuishia hapo tunatoa elimu ya ujuzi na ujasiriamali ambao utawawezesha kujishughulisha kipindi wanapohitimu kidato cha nne," alisema Wilbert.

Alisema wanafanya kazi ya kuanzisha, kuendelea na kukuza biashara zao ikiwamo kuwaelimisha watoto hao juu ya masuala ya uongozi. Alisema kwa mwaka wa fedha 2020/2021 bajeti yao ni Sh. bilioni 19 na hadi sasa wametumia Sh. bilioni 17.

Mkurugenzi huyo alisema kuna wanafunzi ambao wamesomeshwa chuo kwa ngazi ya diploma na cheti katika kozi mbalimbali huku wengine wakifudishwa shughuli za uzalishaji baada ya kuhitimu elimu ya kidato cha nne.

Pia wamelenga kuwafikia watoto katika mikoa yote, lakini hadi sasa wanatekeleza mpango huo katika halmashauri 39 za mikoa ya Morogoro, Dar es Salaam, Iringa, Tanga, Pwani, Mwanza, Shinyanga, Tabora na Singida.

Kwa upande wa mmoja wa wanufaika wa mradi huo kutoka Wilaya ya Chalinze mkoani Pwani, Eva John, alisema kabla ya kupata msaada wa shirika hilo, alikuwa anafanya vibarua vya kubeba maji katika migahawa na uchomaji bagia ili kujipatia fedha za kununua mahitaji ya shule.

Alisema, analishkuru shirika hilo kwa msaada wanaowapa ambao unawasaidia kuwainua kutokana na elimu wanayopewa ya darasani na ujasiriamali.

Eva alisema mazao anayolima anayasafirisha nchini Kenya kwa ajili ya kuuza.

# Miradi maji zaidi ya 200 kuzinduliwa

**Renatha Msungu,** DODOMA

JUMLA ya miradi 281 ya maji yenye thamani ya Sh. trilioni 1.014 inatarajiwa kuzinduliwa na kuwekewa mawe ya msingi katika maadhimisho ya Wiki ya Maji yanayotarajia kuanza Machi 16 hadi 22, mwaka huu.

Maadhimisho hayo mwaka huu yamepangwa kufanyika katika maeneo mbalimbali, kwa watendaji kuwa katika eneo la mradi.

Pia kutakuwa na shughuli nyingine za upandaji miti katika vyanzo vya maji, kuhabarisha na kuhamasisha wananchi juu ya utunzaji wa vyanzo vya maji.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Antony Sanga, alisema maadhimisho hayo yatafanyika kwa kutembelea maeneo mbalimbali ya miradi.

"Lengo kuu la maadhimisho hayo ni kuungana na mataifa mengine duniani katika kutathmini utekelezaji, mafanikio na changamoto zinazojitokeza," alisema.

Alisema maadhimisho hayo yenye kaulimbiu 'Thamani ya Maji kwa Uhai na Maendeleo' watatumia fursa hiyo kuonesha kwa vitendo mafanikio katika sekta ya maji.

Sanga alisema, katika kipindi cha miaka mitano sekta ya maji imeendelea kukua kwa kasi kwa kuboreshwa kwa miundombinu ya maji iliyosababisha kuwafikia wananchi wengi zaidi.

"Tumeweza kuwafikishia maji mijini kwa asilimia 86, wakati kwa vijijini tumewafikia kwa asilimia 53, kwa hiyo inaonesha huduma inahitajika zaidi vijijini," alisema Sanga.

Alisisitiza jamii kulinda vyanzo kwakuwa ni uhai hakuna sababu ya kuyapoteza.

Alisema kuwa katika kuendelea kuboresha mazingira ya upatikanaji maji nchini, mradi mwingine wenye thamani ya Sh. trilioni moja unatarajia kuanza Aprili, mwaka huu.

Alisema, mradi huo uliodhaminiwa na serikali ya India utatekelezwa katika miji 21 nchini.

Pia alisema wizara imebadili sheria ya usimamizi wa maji katika maeneo mbalimbali, awali alikuwa akichaguliwa mtu maarufu kusimamia huduma za maji, lakini hivi sasa anayetakiwa kusimamia awe na taaluma ya ufundi na mtaalamu wa masuala ya maji.

Alisema sababu ni kuepuka uharibifu unaofanywa katika miradi ya maji na msimamizi kushindwa kutoa majibu.

Akizungumzia tatizo la upungufu wa maji jijini Dodoma, alisema inatokana na ongezeko la watu kuhamia na kuitaka jamii kuwa na uvumilivu wakati wakiendelea kutekeleza miradi hiyo ambayo itasaidia kumaliza tatizo lililopo.

"Maji yanatoka kwa mgao, muwe wavumilivu tunatekeleza miradi ya maji ili kumaliza tatizo katika baadhi ya maeneo," alisema Sanga.

Aliwataka wananchi kulinda vyanzo vya maji, kwa kupanda miti, kuboresha mazingira ikiwamo kutoa taarifa wanapoona kuna uharibifu wa mazingira unaochangia upotevu wa huduma hiyo muhimu.





Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, akimkabidhi, Mwenyekiti wa Kikundi kinachojihusisha na shughuli za ukarabati wa madaraja na usafi wa barabara, Magreth Alex, nakala yenye kuthibitisha kupokea fedha kiasi cha Sh. milioni 40 ikiwa ni mkopo wa asilimia 10 unaotokana na makusanyo kwa Halmashauri ya Jiji la Mbeya mwishoni mwa wiki. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Vituo vya kulea yatima vyaonywa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amewaonya baadhi ya wamiliki wa vituo na taasisi za kulelea watoto yatima kuacha tabia ya kutumia sadaka zinazotolewa na wahisani pamoja na wananchi ili kuwasaidia watoto wenye mahitaji kujinufaisha wenyewe.

Chalamila alitoa onyo hilo mwishoni mwa wiki alipotembelea shule jumuishi ya Msingi Mwenge jijini Mbeya, ambayo baadhi ya watoto wenye mahitaji maalum shuleni hapo wanatoka kwenye vituo vya kulelea watoto yatima.

Alisema kuna tabia ya baadhi ya wamiliki wa vituo hivyo kutumia mali zinazotolewa na wadau ili zitumike kuwahudumia watoto kutumika kwa manufaa yao ikiwamo kufungua miradi na shughuli nyingine, jambo ambalo alisema ni dhambi kubwa.

Alisema atafanya ukaguzi kwenye vituo hivyo na akigundua kuwapo kwa ubadhirifu wowote basi vituo hivyo vitafungwa au mhusika kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

"Nadhani kila mmoja wetu hapa ameona hali waliyonayo watoto hawa wenye mahitaji maalum baadhi yao wamesema wanatoka kwenye vituo vya kulelea watoto yatima ukiangalia hali za baadhi yao haziridhisha, naomba vituo hivyo vifanye kazi ya kuwasaidia watoto hawa kama walivyoamua na sio vinginevyo," alisema Chalamila.

Katika hatua nyingine, Chalamila aliwapongeza walimu wa Shule ya Msingi Mwenge kwa jitihada wanazozifanya katika kuwafundisha watoto hasa wenye mahitaji maalum kupitia mpango wa elimu jumuishi kwani matunda yanaonekana.

Alisema watoto hao ambao wako katika hatua mbalimbali za madarasa wanafanya vizuri licha ya hali walizonazo, huku akiwasihi wazazi wa watoto wenye ulemavu kutowaficha ndani badala yake wawapeleke shule ili kupata maarifa.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Aness Mwakaje, alisema jumla ya watoto 1,500 wanasoma shuleni hapo kati yao 90 ni wenye ulemavu na 1,410 ni watoto wa kawaida.

Alisema kupitia mpango wa elimu jumuishi watoto wenye mahitaji maalum wameonyesha mabadiliko ukilinganisha na walivyofika na kuipongeza serikali kuanzisha utaratibu huo. Alisema serikali imejitahidi kuleta vifaa maalum kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalum, lakini kutokana na kuendelea kupokea watoto hao uhitaji unaongezeka pamoja na miundombinu ya majengo yakiwamo madarasa na vyoo.

Mwalimu anayefundisha watoto wenye uoni hafifu, Asteria Silomba, alisema miongoni mwa vikwazo vinavyowakabili ni vifaa vinavyotumika kutokuwa vya kisasa, hivyo aliiomba serikali na wadau wengine kuwasaidia ili kuwafundisha watoto hao na kuelewa kwa urahisi.

# CRS, MUST wagundua mfumo wa kidigitali

**Na Grace Mwakalinga,** MBOZI

SHIRIKA la Misaada la Kanisa Katoliki Relief Services Tanzania (CRS) kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) kupitia kituo cha utafiti na ugunduzi wamefanikiwa kutengeneza mfumo wa kidigitali unaojulikana Fundi Bora.

Lengo ni kuwaunganisha mafundi, wauzaji wa vifaa na wananchi ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za serikali kuhamasisha ujenzi wa vyoo bora na usafi wa mazingira.

Mfumo huo ni moja ya utekelezaji wa mwaka wa tatu wa mradi wa usafi wa mazingira unaotekelezwa na Shirika la CRS kwa kushirikiana na Halmashauri za wilaya za Mbarali, Chunya na Mbeya, Momba na Mbozi.

Mfumo huo umeongeza chachu ya kupatikana kwa huduma katika usambazaji na ununuzi wa bidhaa za usafi wa mazingira kuisaidia jamii kujenga vyoo bora kwa urahisi ulikinganisha na ilivyokuwa awali.

Akizungumza juzi wakati wa kuzindua mfumo huo, Mshauri wa Ufundi wa Shirika la CRS, Mhandisi Godfrey Mpangala, (Fundi bora App) inakutanisha makundi matatu ambayo ni mafundi, wasambazaji wa vifaa vya ujenzi na vya usafi wa mazingira pamoja na watumiaji.

Alisema lengo la kuanzisha mfumo huo kukabiliana na vikwazo vilivyopo kwenye sekta ya utunzaji mazingira kupitia kampeni ya kitaifa ya usafi wa mazingira.

Alisema awali ilikuwa wananchi wanashindwa kupata vyoo bora, hivyo waliamua kuanzisha mfumo huo ambao unapatikana kwenye simu za mkononi kuwaunganisha wanunuzi na watumiaji kupata vifaa vya ujenzi na usafi wa mazingira popote walipo.

"Tumeanzisha chombo ambapo kitawaunganisha watumiaji, watengenezaji na wasambazaji wa vifaa vya ujenzi na usafi wa mazingira kupitia simu za mkononi ambapo popote alipo mwananchi anaweza kupata huduma lengo ni kuifanya jamii kuwa safi na salama ili kuepukana na magonjwa ya milipuko, ikiwamo kipindupindu," alisema Mhandisi Mpangala.

Alisema mradi wa usafi wa mazingira unaoratibiwa na CRS ulisaidia uhamasishaji wa ujenzi wa vyoo bora katika Wilaya za Chunya, Mbarali na Mbeya, lakini tatizo lilikuwa ni namna gani wananchi wengine wanaweza kuwapata mafundi wanaojenga vyoo, hivyo ambao walipatiwa mafunzo na Shirika hilo ndipo wakaanzisha App hiyo iwe rahisi kuwapata.

Alisema matarajio ya mradi huo ni kuzifikia wilaya zote za mikoa ya Songwe na Mbeya ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono kampeni ya usafi wa mazingira.

Aliwaasa mafundi watakaotumia mfumo huo, kuzingatia ubora wa kazi ili kuongeza imani ya wateja na kuongeza kipato huku akiwashauri wateja pia kufanya uchaguzi sahihi wa fundi kwa madai kuwa mfumo huo unatoa uwanja mpana wa kuchagua fundi anayetoa huduma nzuri.

# Chalamila ataka w/biashara wote wapatiwe EFD

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ameishauri serikali kutoa mashine za kielektroniki za kutolea risiti (EFD) kwa wafanyabiashara wote nchini bila kujali kiwango cha mauzo ili kudhibiti ukwepaji kodi unaofanywa na baadhi ya wafanyabiashara kwa kutumia sheria zilizopo.

Alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki alipokuwa anafungua mafunzo kwa maofisa maendeleo ya jamii wa halmashauri za wilaya zote za mikoa ya Njombe na Katavi kuhusu usajili wa vikundi vya kijamii vya huduma ndogo ya kifedha yaliyoandaliwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Aliiahauri Mamlaka ya Mapato (TRA), kubadili mfumo wa ukadiriaji wa kodi kwa wafanyabiashara na kwamba ikiwezekana wasiwe wanatangaza viwango vya mauzo kwa mtu anayestahili kupata msamaha wa kodi.

Alisema sheria za kodi zilizopo zinaweka mianya ya wafanyabiashara kukwepa kodi kwa kuhakikisha mauzo yao hayazidi kiwango kinachotakiwa kulipa kodi.

Alisema Sheria ya Ongezeko la Thamani (VAT) inatoa msamaha kwa mfanyabiashara ambaye mauzo hayafiki Sh. milioni 100 kwa mwaka na sheria ya matumizi ya EFD inatoa msamaha kwa mfanyabiashara ambaye mauzo hayazidi Sh. milioni 14 kwa mwaka. "Sasa wafanyabiashara wanajitahidi mauzo yao yasifike Sh. milioni 14 kwa mwaka ili asipewe mashine hii na wengine wajnajitahidi mauzo yasifike Sh. milioni 100 ili asiingizwe kwenye VAT, sasa nashauri ikiwezekana kila mfanyabiashara anayefanya biashara halali apewe mashine," alisema Chalamila.

Alisema idadi ya wafanyabiashara ambao wanafanya shughuli zao kiujanja ujanja ni wengi na hivyo njia pekee ya kuwadhibiti ni kuhakikisha wanapewa mashine wote bila kujali viwango vya mauzo.

Mkurugenzi wa BoT Tawi la Mbeya, Ibrahim Malogoi, alisema benki hiyo inaendelea na taratibu mbalimbali za usajili wa vikundi vya kijamii vya huduma ndogo ya fedha nchini. Alisema moja kati ya maandalizi ambayo tayari yamefanyika ni pamoja na kutunga kanuni za usimamizi wa huduma hiyo kwa kila ngazi ya vikundi pamoja na kufanya tathmini ya mamlaka ambazo zimekasimiwa kwa vikundi hivyo.

Vilevile, alisema wameandaa mifumo na miongozo ya usajili wa watoa huduma hao wa pamoja na kuta elimu kwa jamii kuhusu sera na sheria ya usimamizi wa huduma ndogo ya fedha.

"Kwa sasa kinachofanyika ni kutoa mafunzo kwa hawa viongozi ambao ndio wanaosajili hivi vikundi ili wanaposajili sheria na miongozo izingatiwe," alisema Malogoi.

Baadhi ya maofisa maendeleo ya jamii walioshiriki mafunzo hayo, waliahidi kuhakikisha vikundi vyote vya kijamii vya huduma ndogo ya fedha ambavyo ni pamoja na Vyama vya Kuweka na kukopa (SACCOS) na Vikoba vinavyoundwa katika maeneo yao vinasajiliwa kwa mujibu wa sheria.

Julius Mwakajila aliwaomba maofisa wa BoT kuendelea kutoa mafunzo hayo ili wafanye kazi kwa ustadi na kuhakikisha sheria zinazingatiwa.



# Rais Mwinyi atoa angalizo nyumba za maafa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewataka wananchi watakaokabidhiwa nyumba za vijiji za maafa zilizojengwa Tumbe Kisiwani Pemba na Nungwi kwa Unguja, kuhakikisha wanazitunza ili zisipoteze mandhari yake.

Rais Dk. Mwinyi alisema nyumba hizo hivi karibuni zinatarajiwa kuzinduliwa kwa upande wa Unguja ikiwamo Pemba, ili wananchi waliokusudiwa waweza kuzitumia.

Aliyaeleza hayo baada ya kumaliza ziara ya kukagua nyumba hizo 15 ambazo zitakaliwa na familia 30, zilizoko katika Kijiji cha Tumbe Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba, wakati wa ziara yake ya siku moja Kisiwani Pemba.

Aidha, Rais Mwinyi aliwashukuru wananchi wa Shehia ya Tumbe kuonyesha kuwa wapo tayari kwa ushirikiano na serikali, huku akisema kwamba changamoto zilizopo katika nyumba hizo zinashughulikiwa ili kumailizika kwa wakati.

"Tumeambiwa kama suala la maji ni changamoto kwa sasa, ila hivi karibuni litamalizika, fedha za fidia nazo zinashuhulikiwa ndani ya wiki hii zinazalishwa na changamoto ya idadi ndogo ya watu wanaohitaji kuwapo hapa nayo inashughulikiwa," alisema. Katika hatua nyingine, Dk. Mwinyi aliwashukuru wafadhili waliojenga nyumba hizo, Emirates Red Creasent ya Falme za Kiarabu kwa kazi kubwa walioifanya, kuhakikisha nyumba hizo wameziwekea na huduma za kijamii ikiwamo, kituo cha afya cha kisasa, shule, msikiti na maduka.

Akizungumzia suala la amani na utulivu, Dk. Mwinyi, aliwataka wananchi wa Unguja na Pemba, kuendelea kudumisha amani iliyopo, umoja na mshikamano, kwani lengo la serikali ya Umoja wa Kitaifa ni kuwaunganisha watu, kwa kuachana na mifarakano iliokuwapo.

"Tumefanya hivi ili kuwaweka wananchi katika hali ya amani, utulivu na usalama ili waweze kupata maendeleo yaliokuwa bora kwa viongozi wao," alisema.

Hata hivyo, Rais Dk. Mwinyi alisema hatua iliyobaki hivi sasa ni serikali kupeleka maendeleo kutokana na kuwapo kwa amani, umoja na mshikamano, huku akitambua kuwa kuna huduma nyingi za kijamii zinazohitajika, ikiwamo afya, maji, elimu barabara na hususan za vijijini, kwani aliwaahidi wananchi wakati wa kampeni kwamba atahakikisha kuwa huduma hizo zinapatikana. Kwa upande wa kinamama aliwahidi kuwa serikali itawapatia mikopo kutoka benki, hivyo wanapaswa kujipanga vyema katika vikundi vyao, kwa kuwapatia mafunzo, mitaji na masoko, kitu watakachopewa kitakuwa na tija nao.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Dk. Khalid Salum Mohamed, alisema nyumba hizo 15 zinazochukua familia 30 kwa wakati mmoja, pia kuna hospitali ya kisasa, soko, maduka 15, msikiti unaochukua watu 350 pamoja na shule yenye vyumba tisa. Dk. Khalid alisema chanzo cha ujenzi wa nyumba hizo ni athari zilizotokea mwaka 2017 za mvua kubwa ya masika, ambayo karibu familia 6500 Unguja na Pemba ziliathirika, lakini watu wa Mwezi Mwekundu walikuja na kushirikiana na serikali kujenga nyumba za kuwasaidia waathirika hao.

Alieleza kuwa waathirika ni wengi, lakini ilionekana familia 385 ambao nyumba zao ingebidi zivunjwe kutokana kuwapo katika maeneo hatarishi, Pemba nzima imeoneka kuna familia 41 nyumba hizo na hao wapate makazi hapo.

`Aidha, alisema kuwa mradi kama huo upo huko Nungwi kwa upande wa Unguja, na kueleza kuwa kwa mujibu wa mkataba serikali imelazimika kutengeneza barabara, kupeleka umeme na maji ambapo kwa upande wa maji tayari visima vitatu wameshachimbwa ila hawakufanikiwa kutokana na uhaba wa maji, lakini hivi sasa wanachimba kingine na kwenda hadi mita 90 na wanatarajia kuyakuta maji.

Kwa upande wa fidia, waziri huyo alisema tayari wameshalipa Sh. milioni 16 na Sh. milioni 11 wanatarajia kuzimaliza ndani ya wiki inayofuata, kati ya milioni 27 walizokuwa wakidaiwa kwa ajili ya fidia.



Fundi mkuu wa jengo la Zanzibar Gender Centre linalojengwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) akitoa maelezo ya ujenzi wa jengo hilo, kwa wanachama wa chama hicho baada ya kumalizika kwa mkutano mkuu, Tunguu Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMANI**

# 'Wanawake hatarini zaidi kupata kisukari'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

DAKTARI bingwa wa magonjwa ya kisukari Hospitali Kuu ya Mnazimmoja, Salama Asaa Ali, amesema wanawake wapo katika hatari zaidi ya kupata ugonjwa huo kutokana na wengi wao kuwa na msongo wa mawazo na uzito mkubwa.

Amesema pamoja na hayo, utafiti unaonyesha wanaume ndio wengi wenye ugonjwa wa kisukari.

Aliyasema hayo juzi wakati akitoa mada kuhusu ugonjwa huo kwa wanachama wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Zanzibar, katika mkutano mkuu wa chama hicho uliofanyia Tunguu nje ya mji wa Zanzibar katika ofisi za chama hicho.

Aliwataka wanawake kuwa na utamaduni wa kufanya mazoezi, kupunguza uzito ili kuepukana na maradhi yasioambukizak ikiwamo kisukari, sindikizo la damu, moyo na saratani.

Alisema lishe bora inasaidia kuepukana na maradhi hayo, hivyo ni vyema kujitahidi kula lishe bora ikiwamo mboga, matunda na kuacha kula vyakula vyenye mafuta na uwanga mwingi.

Alisema wagonjwa wa kisukari Zanzibar wanaongezeka kwa kasi ambapo chanzo kikuu ni uzito wa kupindukia pamoja na umri mkubwa. Akitoa mada kuhusu maradhi ya wanawake na afya ya uzazi, Daktari bingwa wa maradhi hayo kutoka Hospitali ya Mnazimmoja, Ummulkulthum Omar Hamad, alisema matatizo ya wanawake na uzazi ni mengi na hupelekea vifo vya mama na mtoto.

Alisema matatizo ya mama na mtoto hutokea wakati wa kujifungua kutokana na mjamzito kutokwa na damu nyingi, kifafa cha mimba, kisukari na shinikizo la damu.

Alisema vifo vya mama na mtoto kwa sasa vimepungua katika Hospitali ya Mnazimmoja, kutokana na kuongezeka kwa wataalamu wa afya ya uzazi, mama wajawazito kuhudhuria kliniki kwa wakati na serikali kuimarisha huduma za afya ya mama na mtoto.

"Mjamzito anatakiwa kuonanana na mtaalamu wa afya ya uzazi angalau mara nane mpaka kujifungua, hivyo nawasisitiza wajawazito kuhudhuria kliniki kwa wakati," alisema.

# Vijana waaswa mitandao kijamii

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI Mtendaji wa Jumuiya ya Jukwaa la Vijana Zanzibar, Youth Forum (ZYF), Maulid Suleiman, amewataka vijana kutumia mitandao ya kijamii vizuri ili kujiepusha na athari mbalimbali.

Akizungumza katika mafunzo ya kuwajengea uwezo vijana kuhusu kutumia mitandao ya kijamii yaliyofanyika Mjini Unguja, alisema wengi wanatumia vibaya mitandao hiyo na kusababisha kuleta migogoro ndani ya jamii.

Alisema ni vyema kwa vijana hao kutumia mitandao hiyo kwa kutoa taarifa sahihi ambazo zitaleta mafanikio nchini na kufikia malengo yaliyokusudiwa ikiwamo kuelimisha jamii hasa wanaotumia mitandao ya kijamii.

Aidha, alisema lengo la mradi huo ni kuwajengea uwezo taasisi zisizo za kiserikali na ushiriki na utetezi juu ya sera za habari, uhuru wa habari na haki za msingi za binadamu.

Akiwasilisha mada ya matumizi ya mazuri ya mitandao, mwandishi mkongwe wa habari, Dk. Suleiman Seif Omar, alisema kumekuwapo kwa baadhi ya vijana hutumia mitandao ya kijamii kwa kuandika taarifa zisizofuata sheria, jambo ambalo linaweza kuzua vurugu na sitofahamu katika nchi.

Hivyo, alisema kupatiwa mafunzo hayo kutawawezesha vijana kutangaza habari zilizokuwa na ubora na za kweli kwa lengo la kuielimisha jamii.

"Sasa hivi kila mtu mwandishi wa habari, watu wanaitumia taaluma hii wanavyotaka, hivyo ni vyema vijana wakaacha mtindo huu kwani uandishi wa habari ni taaluma na unatakiwa usome na kujua taratibu za kupasha habari badala ya kuivamia taaluma hii," alisema.

Alisema ni vyema kwa vijana wakatumia taratibu na sheria za mitandao ya kijamii kwa kuandika taarifa bila ya kumkwaza mtu.

Washiriki wa mafunzo hayo walisema yatawasaidia kujua sheria za mitandao na kutoa taarifa sahihi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NOTISI YA KUFUNGA KAMPUNI**
**RAMCO GROUP LIMITED KAMPUNI NAMBA 126260**

**NOTISI YA MWEZI DESEMBA**

MWENYEKITI ALIITISHA KIKAO KAMA ILIVYOSTAHILI NA WAHUSIKA WOTE WALIKUWEPO NA MKUTANO HUO ULIFANYIKA TAREHE 07 DESEMBA, MWAKA 2019, SAA 5:00 ASUBUHI NA MAKUBALIANO YAFUATAYO YALIFIKIWA:

WAHUSIKA WALIKUBALIANA KATIKA KIKAO HICHO KWA HIYARI YAO KUWA KAMPUNI HIYO IWE IMEFUNGWA TOKA TAREHE YA KIKAO 07/12/2019 NA HAKUTAKUWA NA BIASHARA YEYOTE AMBAZO ZITAKUWA ZINAENDESHWA KWA JINA AU KATIKA KAMPUNI.

KAMA MWANAHISA YEYOTE ATAKUWA NA LOLOTE JUU YA MAAMUZI HAYA ANATAKIWA AANDIKE BARUA YA KUPINGA MAAMUZI HAYA KWA MSAJILI WA MAKAMPUNI BRELA NDANI YA SIKU 21 KUTOKA TAREHE YA NOTISI HII.
HIVYO BASI MWENYEKITI ALITOA TAMKO KWAMBA HAKUTAKUWA NA BIASHARA YOYOTE ITAKAYOENDESHWA KATIKA KAMPUNI.
MKUTANO ULIFUNGWA MNAMO SAA 8:30 MCHANA.
MAHALI: MWANZA
Tarehe: 07/12/2019
MAIN MOHAMAD NASSER
Mwenyekiti wa Bodi
AHMAD MAIN NASSER
Sekretari wa Bodi

**KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

**JEREMIA MANYAMA NGUKU** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 625 BWR** AINA YA **TOYOTA NOAH VOXY** YENYE **CHASSIS NO AZR600067579** NA **ENGINE NO 1AZ421032 .** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI **KAH/TR/RB/118//2021**

**KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI**

NASSORO SEIF ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI MC 826 AFB. AINA SANLG KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI KAH/TR/RB/103//2021

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**
**IDARA YA UHAMIAJI**

**OMBI LA URAIA WA TANZANIA**

Telegramu: UHAMIAJI
Simu: 027-2751557
027-2752284
E- mail:riokilimanjaro@immigration.go.tz
Kumb. Na. IMM/MS/DN/963/VOL. 11

OFISI YA UHAMIAJI MKOA,
S.L.P 1049
MOSHI
KILIMANJARO
Tarehe: 09/03/2021



**HII NI TAARIFA KUWA:**
**BW MAHAMMAD AARIF ABDULBERG MIRZA**
Ambaye picha yake imeonyeshwa hapo juu, anaomba uraia wa Tanzania kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi .Yeye ni raia wa INDIA na nchi atokayo ni INDIA.
Kazi yake /Shughuli zake ni **IMAMU KATIKA MSIKITI WA AMINA –NJORO, SLP 471 MOSHI**
Ameishi nchini tangu mwaka 2007, Pia amewahi kuishi Mkoa ARUSHA , Mtu yeyete mwenye sababu za kupinga mwombaji asipewe uraia, atume taarifa yake ya maandishi iliyosainiwa kwa:
Kamishna Jenerali wa Uhamiaji,
**S.L.P 512**
**DARE ES SALAAM**

**A/INSP: FULAFU M.SHOMVI**
**KNY: AFISA UHAMIAJI MKOA,**
**KILIMANJARO**

**KUPOTEA KWA CHETI**



**DARIAH GASPAR CLEMENCE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0264/0506** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **BABRO JOHANSON GIRLS SEKONDARI mwaka 2011**. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/OST/RB/142946/2021.**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi**
**NO.70/2021**

Ombi la **JUMANNE KIBWANA DIMOSSO** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **RAJAB SALUM MSUNGI**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe 13/04/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 10/03/2021**

**IN THE DISTRICT COURT OFMOSHI**
**AT MOSHI**
**CIVIL CASE NO.16 OF 2020**

MARY OSWALD CHUWA…….....................1ST PLAINTIFF
VERSUS
1)OSCAR LUCAS KIMARO……….............…1ST DEFENDANT
2)DIDAS RAPHAEL KARIA ......................…2ND DEFENDANT
3)THE HERITAGE INSURANCE COMP.LD…..3RD DEFENDANT

**NOTICE OF MENTION/HEARING**

**TO: OSCAR LUCAS KIMARO( DEFENDANT)**
Take Notice that the above case has been fixed for mention in the District Court of Moshi at 1st the day of April 2021.
You are hereby ordered to appear in person or by advocate of agent dully authorized to do so and you are directed to produce on that day any document under which you intend to rely in support of your case.
**TAKE FURTHER NOTICE** that, default of your appearance on that day afore mentioned the court will proceed with the matter in your absence.
Given under my hand and seal of this Court this 12th day of March, 2021
**PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE**
**MOSHI**

**Uza,**
**Chenye Thamani**
**Kubwa Kwa Kutangaza**
**Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# DRC yaahirisha uzinduzi AstraZeneca

**Kinshasa, DRC**

JAMHURI ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), imeahirisha kampeni ya chanjo ya AstraZeneca dhidi ya Covid-19, ikifuata mfano wa nchi nyingine kadhaa zilizochukua kama hiyo.

Hayo ni kwa mujibu wa taarifa ya serikali ya nchi hiyo.

Serikali ya nchi hiyo ilipokea dozi milioni 1.7 ya chanjo inayotengenezwa na kampuni ya AstraZeneca ya Uingereza na Sweden na ilitarajiwa kuanza zoezi la kuwachanja watu leo.

''Tumeamua kuchelewesha tarehe ya uzinduzi wa chanjo hii nchini Congo, kama hatua ya tahadhari.''

Alisema Waziri wa Afya, Eteni Longondo, katika taarifa iliyotolewa mjini Kinshasa.

Denmark, Norway, Bulgaria na Iceland zilisimamisha matumizi ya chanjo ya AstraZeneca wiki hii, kama hatua ya tahadhari kufuatia hofu kuwa huenda ilikuwa ikisababisha kuganda kwa damu.

India kwa upande mwingine ilitangaza Jumamosi kwamba, inaanzisha uchunguzi wa kina kujua athari za baada ya chanjo dhidi ya Covid-19.

Hata hivyo, Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), lilisema hakuna uhusiano wowote kati ya chanjo ya AstraZeneca na kuganda kwa damu na limesisitiza kuwa chanjo hiyo ni salama.

''Ndiyo, tunapaswa kuendelea kuitumia chanjo ya AstraZeneca,'' alisema Msemaji wa WHO, Margaret Harris, akisema kuwa wasiwasi wowote wa usalama wa chanjo hiyo lazima ufanyiwe uchunguzi.

Kampuni ya AstraZeneca ilikanusha madai dhidi ya chanjo yake, ikisema hakuna ushahidi wowote kuwa wanaoipokea wanakabiliwa na hatari ya kuganda kwa damu.

Waziri wa Afya, DRC, alisema tarehe mpya ya kuanzisha kampeni ya chanjo itatangazwa baada ya kupata majibu ya uchunguzi utakaofanywa na wataalamu wa kitaifa na wa kimataifa.

Maofisa wa afya nchini Norway wamesema visa vitatu vya kuganda kwa damu na kuvuja damu katika ubongo viliripotiwa miongoni mwa watu wa umri mdogo waliopata dozi ya chanjo hiyo ya AstraZeneca, ingawa hawawezi kuthibitisha kuwa matatizo hayo yametokana na chanjo hiyo.

''Ni jukumu la Kitengo cha Dawa cha Norway kuzichunguza matukio haya yanayodhaniwa kuwa athari za chanjo, na kuchukua hatua muafaka,'' alisema Geir Bukholm, Mkurugenzi wa Taasisi ya Norway ya Afya ya Jamii anayehusika na kudhibiti magonjwa ya kuambukiza.

Msemaji wa kampuni ya AstraZeneca, aliliambia Shirika la Habari la AFP, kwamba 'usalama wa chanjo umethibitishwa na utafiti wa kina wa ngazi ya tatu, na wadau waliolinganisha data zao, walisema bayana kuwa chanjo hiyo inakubaliwa na mwili wa binadamu.

***DW***



Waandamanaji wanaopinga mapinduzi ya kijeshi wakiwa wamembeba aliyejeruhiwa baada ya vurugu kati yao na polisi, mjini Yangon, nchini Myanmar, jana. **PICHA/AP**

# Marekani kutoa makazi raia Myanmar

**Washington, MAREKANI**

RAIA wa Myanmar wanaoishi Marekani watapewa vibali vya makazi ya muda nchini humo.

Waziri wa Usalama wa Ndani wa Marekani, Alejandro Mayorkas, alikumbusha kwamba jeshi lilichukua utawala Februari Mosi, mwaka huu na kutangaza kuwa wakazi wa Myanmar nchini Marekani watapewa vibali vya makazi ya muda.

Katika taarifa yake, Waziri Maorkas alisisitiza kuwa vibali hivyo vitadumu kwa miezi 18 na kwamba mapinduzi hayo yalifanya hali za kibinadamu kuwa mbaya na kusababisha ugumu kwa raia wa Myanmar wanaoishi Marekani kurudi katika nchi zao.

Jeshi la Myanmar lilipindua utawala baada ya vikundi vya kisiasa vilivyo karibu nao kudai kwamba kulikuwa na udanganyifu katika uchaguzi uliofanyika Novemba 8, mwaka jana na mvutano wa kisiasa kuongezeka.

Jeshi lilitangaza hali ya hatari kwa mwaka mmoja na kukamata maofisa na viongozi wa chama tawala akiwamo Aung San Suu Kyi.

***TRT***

**Katika taarifa yake, Waziri Maorkas alisisitiza kuwa vibali hivyo vitadumu kwa miezi 18 na kwamba mapinduzi hayo yalifanya hali za kibinadamu kuwa mbaya na kusababisha ugumu kwa raia wa Myanmar wanaoishi Marekani kurudi katika nchi zao.**

# Video wanafunzi kutekwa yaibuka

**Kaduna, NIGERIA**

WANAFUNZI waliotekwa nyara katika Jimbo la Kaduna Kaskazini Magharibi mwa Nigeria, siku mbili zilizopita, wameonyeshwa kwenye mkanda wa video huku kukiwa na madai ya fidia katika kituo cha televisheni nchini humo jana.

Video hiyo ilionyesha picha za kutisha ikiwa ni pamoja na wasichana hao wakipiga kelele wakati wanachapwa na watekaji huku picha nyingine zikionyesha wasichana wengine wakiwa wameketi sakafuni wakiwa nusu uchi.

Alhamisi wiki iliyopita, watu wenye silaha waliwateka nyara wanafunzi 39, kati yao wasichana 23 na wavulana 16 wa Chuo cha Shirikisho cha Masuala ya Misitu katika jimbo la Kaduna.

Aidha picha nyingine za video hiyo, zilimwonyesha mwanaume mmoja aliyejitambulisha kwa jina la Benson Emmanuel, akiomba serikali kuwasaidia, na kuonya kuwa juhudi za kuwaokoa zitaweka maisha yao katika hatari.

Vyombo vya habari viliripoti kuwa wazazi na wanafunzi wengine waliwatambua wanafunzi waliotekwa.

Hapo jana Rais Muhammadu Buhari, aliliamuru jeshi kuhakikisha linawarudisha katika familia zao, wanafunzi wote waliotekwa.

***DW***

# LEWANDOWSKI AWEKA REKODI BUNDESLIGA




**MUNICH, Ujerumani**

ROBERT Lewandowski amejivuta hadi nafasi ya pili kwenye orodha ya wafungaji bora wa wakati wote wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

Lewandowski aliingia kwenye rekodi hiyo wakati Bayern Munich ikipata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Werder Bremen, Jumamosi.

Nyota huyo wa kimataifa wa Poland ameifikia rekodi ya mabao 268 iliyowekwa na Klaus Fischer wakati alipokuwa kwenye orodha ya wafungaji wa Bayern pamoja na Leon Goretzka na Serge Gnabry.

Lewandowski anahitaji mabao mengine 97 kufikia rekodi ya gwiji wa Bayern, Gerd Muller aliyefunga mabao 365.

Werder walikuwa na matumaini ya kuwapa presha mabingwa hao, wakati Ludwig Augustinsson alipofunga bao la uongozi, lakini mwisho wa siku wakajikuta wakiangukia pua.

## Guardiola ampigia debe Stones kuitwa England



**LONDON, England**

JOHN Stones anastahili kuitwa timu ya Taifa ya England, kwa mujibu wa kocha wa Manchester City, Pep Guardiola.

Mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 26, alifunga bao la ufunguzi wakati City ikiibuka na ushindi wa 3-0 dhidi ya Fulham, juzi Jumamosi kwenye Ligi Kuu England.

Stones amekuwa na kiwango cha kuvutia kwenye ligi katika miezi ya hivi karibuni, na hivyo kuibua mazungumzo ya kutakiwa kuitwa kwenye kikosi cha England kwa mara ya kwanza tangu Novemba 2019.

Alipoteza nafasi yake kwenye kikosi cha City, lakini msimu huu amepambana na kurudi kuwa mmoja wa wachezaji muhimu, akicheza mechi 25 kwenye mashindano yote, ikiwamo kuanza katika mechi 18 za ligi.

Kocha wa England, Gareth Southgate atatangaza kikosi cha England wiki hii kwa ajili ya mechi za kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya San Marino, Albania na Poland.

"Anastahili," alisema Guardiola. "Bilashaka Gareth Southgate anajua vizuri zaidi kuliko mimi, kinachosubiriwa ni jambo la kuona tu kama itatokea, ningekuwa mimi ningemuita kikosi cha timu ya taifa.

"Alikuwa na kiwago bora kabisa, kwa upande wangu bao alilofunga lilikuwa bora kabisa."

Stones amecheza mechi 39 za timu ya taifa kwa jina lake tangu alipoitwa kwa mara ya kwanza mwaka 2014.

Alikuwa sehemu ya kikosi cha England kwenye Kombe la Dunia mwaka 2018, akifunga mara mbili kwenye ushindi wa 6-1 dhidi ya Panama.

## Simeone: Mbio za ubingwa LaLiga ngumu

**MADRID, Hispania**

DIEGO Simeone amedai kwamba, Real Madrid na Barcelona hazipo tayari kupoteza tena msimu huu, huku akisema ni kawaida kwa timu yake ya Atletico Madrid kuhisi presha.

Vinara hao wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, walilazimishwa suluhu Jumamosi, wakati waliposhindwa kuwafunga Getafe waliokuwa na wachezaji 10 uwanjani.

Golikipa David Soria alikuwa kwenye kiwango bora kwa Getafe, akiokoa hatari saba likiwamo shuti la Moussa Dembele - huku Luis Suarez akigongesha mwamba.

Matokeo hayo yameifanya Atleti kuongoza msimamo kwa tofauti ya pointi sita dhidi ya wapinzani wao wa jiji moja Madrid waliopo nafasi ya pili, lakini Barca wanaweza kupunguza pengo la pointi hadi nne dhidi ya kikosi hicho cha Simeone kama watawafunga Huesca leo, Jumatatu.

Karim Benzema alifunga mabao mawili kuiwezesha Madrid kupata ushindi dhidi ya Elche mapema Jumamosi, na Simeone anaamini bado mbio za ubingwa ni ngumu.

"Tulikuwa na wazo la kushinda tena na kuendelea kuongoza kwa pointi nyingi," alisema akiwambia waandishi wa habari.

"Kipindi cha kwanza hakikuwa kizuri, mchezo haukwenda sawa, hakukuwa na mawasiliano mazuri. Katika kipindi cha pili timu iliimarika na mwishoni tulikuwa na nafasi zaidi za kufunga."

Alipoulizwa kama Atleti inahisi presha kwenye mbio za ubingwa, Simeone alijibu: "Ni kawaida, kwa karibia msimu mzima tumekuwa wa kwanza."

## HABARI MICHEZO

### NEYMAR AKARIBIA KURUDI DIMBANI PSG

**PARIS, Ufaransa**

MAURICIO Pochettino amebainisha kwamba, Neymar anakaribia kurudi kwenye kikosi cha Paris Saint-Germain.

Kocha huyo wa PSG hakutaja muda maalumu wa Neymar kurejea kwenye kikosi hicho wakati akizungumzia kuelekea mchezo wao wa jana Jumapili dhidi ya Nantes, ambao wapo kwenye nafasi ya 19 katika msimamo wa Ligue 1.

Alipoulizwa kuhusu lini Neymar atarudi uwanjani, Pochettino alielezea: "Nafikiri nilisema kwamba alikuwa na nafasi ya kurudi kwenye mchezo wa pili dhidi ya Barcelona.

"Lakini pia tulijua kuwa hatuwezi kupanga muda maalumu kwa kurudi kwa mchezaji ambaye yupo majeruhi, kwa sababu ni vigumu kutabiri.

"Alifanya mazoezi na kikosi leo (juzi), alionekana kuimarika zaidi na tuna matumaini atarudi kwenye kikosi haraka sana.

"Anaonekana kuwa tayari kurudi uwanjani, hivyo tunasubiri muda mwafaka kuweza kujiunga na kikosi chetu."

### UNITED, CHELSEA ZAPIGANA VIKUMBO KWA MANCINI

**ROME, Italia**

MLINZI wa AS Roma, Gianluca Mancini, anawaniwa na timu kubwa mbili ambazo zinashiriki Ligi Kuu England, Manchester United na Chelsea, kwa mujibu wa Sky Sport Italia.

Beki huyo mwenye umri wa miaka 24, amekuwa na msaada mkubwa ndani ya timu hiyo inayoshiriki Serie A na ameweza kutimiza majukumu yake kwa kuilinda timu hiyo kucheza mechi saba bila kufungwa na ametupia mabao manne.

Sky Sport Italia imeripoti kwamba, Man United na Chelsea zipo tayari kumlipa nyota huyo mkwanja mrefu ili ziweze kupata huduma yake.

Ushindi wa Roma wa mabao 3-0 dhidi ya Shakhtar Donetsk kwenye Ligi ya Europa katika hatua ya 16-bora umedhihirisha uwezo wa nyota huyo, ambaye dau lake linatajwa kuwa pauni milioni 27.

Kocha wa Man United, Ole Gunnar Solksjaer anatajwa kuweka mpango wa kuisaka saini yake ili kuongeza nguvu ndani ya kikosi chake ambacho kipo kwenye mazungumzo na nyota wao, Eric Bailly ili kuongeza mkataba mpya.

Pia Solskjaer anahitaji kumwongezea mkataba beki wao wa kati Harry Maguire, huku United pia ikitajwa kuingia kwenye rada za kuisaka saini ya nyota wa RB Leipzing, Ibrahim Konate na Jules Kounde wa Sevilla.



# ZIDANE

## ASHIKWA KIGUGUMIZI RONALDO KURUDI REAL MADRID

**MADRID, Hispania**

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, ameshindwa kukanusha tetesi za mshambuliaji wa zamani wa klabu hiyo, Cristiano Ronaldo kurejea katika timu hiyo.

Katika mkutano na vyombo vya habari, Zidane alisema Ronaldo ni mchezaji aliyefanya makubwa katika timu hiyo, lakini hawezi kuzungumza chochote kwa sasa.

"Mnajua Cristiano Ronaldo ana maana gani kwenye klabu hii, alichofanya hapa, upendo tulioku-wa nao kwake, na alichofanya hapa ni kitu kikubwa sana.

"Lakini kwa sasa ni mchezaji wa Juventus, na anafanya vizuri sana kule, siwezi kusema chochote, vitu vingi vinasemwa sana, lakini lazima uheshimu haya mambo," alisema.

Ronaldo kwa sasa ana miaka 36, akiwa anaelekea kwenye miezi 12 ya mwisho katika mkataba wake na Juventus na anatajwa kurejea Real Madrid.

Baada ya Juventus kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, uvumi ulienea kwenye vyombo vya habari vya Italia, kwani Ronaldo ataondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu huu.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Ronaldo mwenyewe ameonyesha nia ya kutaka kurejea nchini Hispania katika Klabu ya Real Madrid.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# VAN DIJK, GOMEZ KUIKOSA EURO 2020

**Si maamuzi yangu, lakini kiukweli taarifa nilizo nazo kwa sasa ni ngumu sana kwao kucheza mashindano hayo...**

**LIVERPOOL**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp anaamini "itakuwa ngumu" Virgil van Dijk au Joe Gomez kucheza michuano ya Mataifa ya Ulaya, Euro 2020, mwaka huu.

Michuano ya Euro 2020, ilihamishiwa mwaka huu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, na hivyo itaanza Juni 11.

Nyota wa Uholanzi, Van Dijk amekuwa nje ya dimba tangu Oktoba baada ya kuumia goti, wakati mlinzi wa England, Gomez amekuwa nje ya uwanja tangu Novemba kutokana naye kuumia goti.

Klopp amesema hatarajii van Dijk au Gomez kuwa tayari kwa ajli ya mashindano hayo baada ya kuumia huko.

"Si maamuzi yangu, lakini kiukweli, taarifa nilizo nazo kwa sasa ni ngumu sana kwao kucheza mashindano hayo," alisema.

"Tuna matumaini kwamba, watakuwa tayari na sisi wakati wa maandalizi ya msimu mpya.

"Lakini kwa sasa, sidhani kama kuna uwezekano wa wao kurejea dimbani, sisi matumaini yetu ni kuwa nao kwenye maandalizi ya msimu mpya, lakini sio sasa kama ambavyo wengi wanadhani na hivyo ndio tunavyotumaini.

"Kwa upande wa Joel (Matip) naye ni kama sawa tu, hawezi kucheza kwenye michuano ya Euro."

Uholanzi imepangwa kundi moja na Ukraine, Austria na Macedonia kwenye Kundi C, huku England wakipangwa Kundi D na Croatia, Scotland na Jamhuri ya Czech.

## KWA UFUPI

### UNITED SASA WAMTAKA POPE

MANCHESTER United imemwongeza golikipa wa Burnley, Nick Pope katika orodha ya wachezaji inaohitaji kuwasajili, ingawa wanaweza kukabiliwa na ushindani kutoka Tottenham kwa nyota huyo wa England mwenye umri wa miaka 28. ***(Daily Star on Sunday)***

### PIRLO NA UVUMI WA RONALDO

KOCHA wa Juventus, Andrea Pirlo amesema ni "kawaida kuwa na uvumi" kuhusu majaliwa ya mshambuliaji wa kimataifa wa Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 36, baada ya kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Football Italia)***

### OLE KUPEWA MKATABA

MANCHESTER United inapanga kumpa kocha, Ole Gunner Solskjaer mkataba mpya, huku wa sasa ukiwa unaingia kwenye mwaka wake wa mwisho baadaye mwezi huu. ***(Sunday Mirror)***

### POGBA KWENYE RADA PSG

KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba, yupo kwenye rada za kuwaniwa na Paris St-Germain kwenye usajili wa kipindi cha majira ya joto na mabingwa hao wa Ligue 1 wameshawasiliana na wakala wa nyota huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 27. ***(Foot Mercato)***

### WIJNALDUM AKARIBIA BARCA

MKATABA wa kiungo wa Liverpool, Georginio Wijnaldum na klabu hiyo unamalizika kipindi cha majira ya joto na sasa nyota huyo mwenye umri wa miaka 30 raia wa Uholanzi ana asilimia 95 ya kutua Barcelona. ***(Football Insider)***

### RONALDO AFUNGUKA MADRID

CRISTIANO Ronaldo, ambaye amehusishwa na mpango wa kurudi Real Madrid, amesema kwa sasa akili yake ni kumaliza msimu vizuri na Juventus. ***(Mail on Sunday)***

### KOEMAN KUONDOLEWA BARCA

BARCELONA inapanga kumwondoa kocha wake, Ronald Koeman baada ya Joan Laporta kuwa rais wa klabu hiyo kwa mara ya pili. ***(Sport)***

### ALABA AGOMBEWA ULAYA

CHELSEA na Manchester City zipo kwenye mbio moja ya kuwania saini ya mlinzi wa Austria, David Alaba, ambaye mkataba wake na Bayern Munich unamalizika mwishoni mwa msimu huu, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 akihusishwa na Barcelona na Real Madrid. ***(Daily Star on Sunday)***

### SPURS WAMTAKA VESTERGAARD

KLABU ya Tottenham Hotspur inaangalia uwezekano wa kumsajili mlinzi wa kati wa Southampton, Jannik Vestergaard mwenye umri wa miaka 28 raia wa Denmark, ambaye mkataba wake unamalizika mwaka 2022. ***(Sunday Mirror)***

### AANHOLT AWANIWA LEEDS

LEEDS United inataka kumsajili mlinzi wa pembeni wa Uholanzi, Patrick van Aanholt mwenye umri wa miaka 30, ambaye mkataba wake na Crystal Palace unamalizika kipindi cha majira ya joto. ***(Sunday Mirror)***

### SARR KURUDI CHELSEA

MLINZI wa Ufaransa, Malang Sarr mwenye umri wa miaka 22, anatarajia kupambana kupata namba kwenye kikosi cha kwanza cha Chelsea, wakati atakaporudi kwenye timu hiyo akitoka kucheza kwa mkopo mrefu kule Porto. ***(L'Equipe, via Metro)***

HABARI MICHEZO

# NDAYIRAGIJE, BARAZA WANUKIA KUMRITHI MAXIME KAGERA SUGAR

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI uongozi wa Klabu ya Kagera Sugar ukieleza kuwa bado unaendelea na mchakato wa kumpata kocha mkuu atayerithi mikoba ya Mecky Maxime waliyemtimua kazi, makocha wawili wa kigeni Mkenya Francis Baraza na Mrundi Etienne Ndayiragije ndio wanaopewa nafasi kubwa, imefahamika.

Kagera Sugar ambayo kwa sasa ipo mikononi mwa Kocha Msaidizi, Peter Manyika, ilimtimua Maxime wiki mbili zilizopita baada ya kutofurahishwa na mwenendo wa matokeo ya timu hiyo kwenye Ligi Kuu Bara.

Hata hivyo, awali uongozi wa klabu hiyo ulionyesha nia ya kuitaka huduma ya Baraza kabla ya timu yake ya Biashara United ya mjini Musoma, kuibuka na kusema itapigana kufa kupona kuhakikisha kocha huyo haondoki. Lakini sasa, mbali na Baraza pia aliyekuwa Kocha Mkuu wa timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, Ndayiragije naye anatajwa kuwa katika rada za miamba hiyo inayotumia Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.


Hata hivyo, Ndayiragije ni miongoni mwa makocha wanaohusishwa na kutakiwa kurithi mikoba ya Mrundi mwenzake, Cedric Kaze, ambaye Machi 7, mwaka huu, alitimuliwa nafasi ya ukocha mkuu ndani ya Klabu ya Yanga baada ya sare ya bao 1-1 dhidi ya Polisi Tanzania katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Lakini kwa sasa upepo unaonekana kubadilika Yanga na kuna kila dalili ikatupilia mbali uwezekano wa kumnasa Ndayiragije na kuajiri kocha Mzungu kama ilivyo kwa watani zao, Simba wanaonolewa na Mfaransa Didier Gomes.

Hata hivyo, Katibu Mkuu wa Kagera Sugar, Ally Masoud, amemwambia mwandishi wetu kuwa mchakato wa kumpata kocha mpya bado unaendelea ikiwa ni pamoja na kufanya mazungumzo na makocha mbalimbali.

"Mambo yakiwa sawa tutawafahamisha mashabiki wetu muda si mrefu, ila bado tunaendelea na mazungumzo," alisema.

KASHINDA...




Mshindi wa bonasi ya Jackpot ya SportPesa, Emmanuel Malima (katikati), mkazi wa Tabata, Dar es Salaam, akionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 13. 7 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya wiki iliyopita ya SportPesa ambayo kwa sasa imefikia Sh. 506,046,080. Kutoka kushoto ni wachezaji wa Klabu Simba ambayo inadhaminiwa na SportPesa, David Kameta 'Duchu' na Meddie Kagere, wakati kulia ni Chris Mugalu na Rally Bwalya ambao mwishoni mwa wiki walihudhuria hafla hiyo fupi ya Malima kukabidhiwa hundi yake. **PICHA: SPORTPESA**

# Mbio za Wanawake zafana Dar

**Na Mwandishi Wetu**

MBIO za Wanawake Tanzania, jana zilifana kwenye viwanja vya Chuo Kikuu Dar es Salaam huku washindi watatu wakipata medali baada ya kushinda.

Mbio hizo ziliwahusisha wanawake pekee lengo likiwa ni kukutana na kutengeneza jukwaa la wanawake wa rika, nyadhifa tofauti na kikubwa kujadili uzoefu na changamoto mbalimbali wanazopitia.

Katika mbio hizo washindi watatu walijizolea medali pamoja na vyeti vya ushiriki, mshindi wa kwanza akiwa ni Rebeka Machege, wa pili Annika Stanley na watatu, Beatrice Edward waliokimbia kilometa 10.

Mratibu wa mbio hizo, Pili Hussein, alisema malengo yao yametimia kwa asilimia kubwa, na kubwa lilikuwa ni kukutana wanawake na kubadilishana mawazo tofauti na mbio hizo.

Pili alisema amefurahishwa na mwitikio mkubwa wa wanawake wa rika na nyadhifa tofauti waliojitokeza kwa wingi katika mbio hizo. "Kama mratibu wa mbio hizi, nimefurahishwa na mwitikio mkubwa wa wanawake waliojitokeza katika mbio hizi ambazo niliziandaa kwa lengo la kukutana na kubadilishana mawazo.

"Lakini nichukue nafasi hii kuwapongeza washindi wa mbio hizi ambazo washindi wamepata medali pamoja na vyeti vya ushiriki," alisema Pili.

## Nahodha Simba amfuata Msuva

**Na Adam Fungamwango**

NAHODHA wa vinara wa Ligi Kuu ya Wanawake nchini Tanzania, Simba Queens, Mwanahamisi Omari, ameondoka nchini kwenda kujiunga na klabu ya Chabab Atlas ya nchini Morocco, ambayo ni klabu ya Ligi Kuu.

Mwanahamisi ambaye ametua nchini humo kama ilivyo kwa Mtanzania, Simon Msuva anayecheza Ligi Kuu ya wanaume akiitumikia Wydad Casablanca, amekwenda kucheza soka la kulipwa baada ya kukipiga hapa nchini kwa kipindi cha miaka 10 na msimu uliopita aliiongoza timu hiyo kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara kwa wanawake.

"Nimecheza ligi nyumbani kwa muda mrefu, takriban miaka tisa au kumi. Ni muda sasa wa kutafuta changamoto mpya, kujijengea uzoefu nikiwa na timu nyingine nje ya nchi," alisema nahodha huyo anayevaa jezi namba saba mgongoni na alipewa, akifananishwa uchezaji wake na Emmanuel Okwi, mchezaji wa zamani wa Simba ambaye aliporejea tena kwenye timu hiyo kwa mara ya pili alipewa jezi yenye namba hiyo.

Mchezaji huyo ametoa shukrani kwa Mwekezaji wa Simba, Mohamed "Mo" Dewji, Ofisa Mtendaji Mkuu Barbara Gonzalez, mlezi wa Simba Queens, Fatema Dewji na Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Salim, Abdallah 'Try Again', kwa kumlea kwenye kikosi hicho hadi kufanikisha kupata dili hilo.

## JKU sasa yapigana kujinasua kushuka

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA wa Timu ya JKU Omar Khamis "Matu", amesema licha ya timu hiyo kuendelea kupata matokeo ambayo hayaridhishi, bado anaamini haiwezi kushuka daraja.

Akizungumza na gazeti hili jana, kocha huyo, alisema tangu kuanza msimu huu timu hiyo hajafanya vizuri vya kutosha, hivyo kilichobaki ni kujilinda ili kubaki Ligi Kuu msimu ujao.

Alisema nguvu zake zote kwa sasa anazielekeza katika kuiokoa timu hiyo isihuke daraja baada ya kushindwa kufikia malengo ya kuunyakuwa ubingwa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu. Alisema kitu kikubwa kinachohitajika ni kuwarejesha wachezaji mchezoni pamoja na viongozi wa timu hiyo kutokata tamaa katika michezo iliyobaki.

"Nguvu kubwa tunazielekeza kuhakikisha hatushuki daraja, hili tutafanikiwa endapo wachezaji tutawarejesha mchezo ili tufanye vizuri michezo iliyobaki," alisema baada ya juzi kulazimishwa sare tasa dhidi ya timu ya Chuoni katika Uwanja wa Amaan.

# Michezo

Jumatatu Machi 15, 2021

Nipashe




VAN DIJK, GOMEZ KUIKOSA EURO 2020

HABARI UK 22

MNAHESABU?...



Wachezaji wa Simba wakiwa mazoezini. **PICHA: MAKTABA**

# GOMES AIPATIA DOZI SIMBA YA AL-MERRIKH

## ●●●Kumaliza hesabu za Al Ahly na AS Vita mapema huku akiwabadilishia kikosi Wasudan hao kwa...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI kesho miamba ya soka nchini, Simba ikishuka Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kuikaribisha Al-Merrikh kwenye mechi ya raundi ya nne hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa mabingwa hao wa Tanzania, Didier Gomes, amepata dozi ya kuwamaliza Wasudan hao.

Simba ambayo inaongoza msimamo wa Kundi A linalojumuisha mabingwa watetezi, Al Ahly ya Misri, AS Vita ya DR Congo na Al-Merrikh, ikiwa na pointi saba kileleni, itavaana na Wasudan hao ikiwa na kumbukumbu ya kulazimishwa sare tasa kwenye mechi ya awali nchini Sudan.

Hata hivyo, Gomes amesema katika mchezo huo watashambulia kwa kasi zaidi huku wakijilinda kwa pamoja tofauti mechi ya awali timu hizo zilipokutana Sudan wiki mbili zilizopita.

Gomes alimwambia mwandishi wetu kuwa kuna kila sababu ya kubadili mbinu tofauti na walivyocheza mchezo uliopita ugenini ili kuweza kuibuka na pointi zote tatu nyumbani.

Alisema maandalizi ambayo wanayafanya yana tofauti na anatarajia kuboresha kikosi kwa kubadili baadhi ya wachezaji watakaoanza kutoka kikosi kilichowavaa Wasudan hao kwenye mchezo wa awali.

Kocha huyo raia wa Ufaransa, alisema ili kupata matokeo chanya lazima kuivaa Al-Merrikh na mbinu mbadala tofauti walivyokutana nao ambapo walitumia mfumo wa kujilinda zaidi na kufanya mashambulizi ya kushtukiza. Alisema nidhamu ya ukabaji ni muhimu huku wakianzia mashambulizi nyuma, na kila mchezaji atakuwa na jukumu zaidi ya moja uwanjani hususan wakati timu inapopoteza mpira.

"Utakuwa ni mchezo mgumu kwa kila upande, lakini muhimu sana kwetu kwa sababu tukishinda utarahisisha kazi yetu ya kwenda kucheza hatua inayofuta, wote tuliwaona Al-Merrikh jinsi ambavyo wanacheza kwa kasi na nguvu kubwa, natumaini kila mmoja sasa analitambua hilo," alisema.

Endapo Simba itashinda mechi hiyo, itafikisha pointi 10, ambazo zitakuwa kaa la moto kwa Al Ahly na AS Vita zenye alama nne kila moja wakati huu ambao nazo zitakutana DR Congo kesho baada ya mechi ya awali kutoka sare nchini Misri.

Kimahesabu Simba ikishinda, itakuwa ikihitaji sare moja tu ili kujihakikishia hatua ya robo fainali bila kujali matokeo yoyote kati Al Ahly na AS Vita kesho.

Mchezo huo wa Simba kesho utachezwa bila mashabiki kutokana na Shirikisho la Soka Afrika, (Caf) kutoa zuio hilo.

# MWAMBUSI AANIKA MIKAKATI YANGA SC

**Na Saada Akida**

KAIMU Kocha Mkuu wa Yanga, Juma Mwambusi, amesema mikakati aliyokwenda nayo kwa sasa ni kuhakikisha wanapambana kutafuta pointi katika kila mechi iliyopo mbele yao iwe ya Ligi Kuu Tanzania Bara ama Kombe la FA.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mwambusi alisema kazi kubwa ambayo wanaifanya kwa sasa ni kuhakikisha wanaendelea na mazoezi ya kuchezea mpira na washambuliaji kuwa makini hasa nafasi wanazozitengeneza.

Alisema malengo makubwa waliyokuwa nayo kwa sasa ni kupambana kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika kila mechi iliyo mbele yao ya ligi pamoja na Kombe la FA.

**"Wiki hizi tatu za mapumziko nitahakikisha kwa wachezaji waliokuwapo kwa sasa nawapa maelekezo na kufanyia kazi upungufu ambao umekuwa ukijitokeza kikosini, mimi si mgeni na Yanga, hivyo nina imani tutafanya vizuri," alisema Mwambusi.**

Alisema suala la mbinu mbadala za ushindi litafanyika baada ya wachezaji waliopo kwenye majukumu ya timu ya taifa, kurejea klabuni.

Mwambusi alisema hawezi kuzungumzia suala la ubingwa ila wanahitaji kupambania timu hiyo kupata matokeo mazuri kwa kila mechi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002